Pambazuko

Toleo Namba 089 | Jumatatu, Septemba 16-22, 2024

Fuatilia mfululizo wa makala za Afcon kila Jumatatu ukurasa wa 33 | Gazeti Maalum la Afcon 2027

Mapya, magumu mauaji ya Kibao

- Aliuawa ndani ya saa sita, atobolewa macho
- Binti yake aeleza kinachotakiwa na familia



Habari Uk. 6&7

Wachumi waeleza mazito Dira ya Maendeleo 2050

WATAALAM wa uchumi na biashara wamesema ufanisi wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050, inategemea zaidi ushirikiano wa sekta binafsi na

Habari Uk. 34





Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi (kushoto), akiteta jambo na Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu wakati wa Kongamano la Tano la Ekaristi Takatifu Kitaifa, lililofanyika Jijini Dar es Salaam jana. (Na Mpigapicha Wetu)

Wanasubiri nini kujiuzulu?

- Maaskofu, wanazuoni, wananchi washinikiza

KUTEKWA, kuteswa na hatimaye kuuawa kwa Mkuu wa Usalama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mohammed Ali Kibao, kumeibua shinikizo la kutaka wenye dhamana ya vyombo vya ulinzi na usalama, kujiuzulu.

Uk. 14

Soma Ndani

Isaka: Sina uvumilivu kwenye rushwa



Soma zaidi Uk. 20

Sifa za anayefaa kuongoza Tanzania

Habari Uk. 4

Tahariri/Katuni

Ianzishwe kurugenzi huru kuchunguza Polisi

MACHI 25, mwaka huu, gazeti la Pambazuko liliandika tahariri ambayo ilimtaka Rais Samia Suluhu Hassan kuridhia kufanyika kwa mageuzi makubwa ndani ya Jeshi la Polisi.

Mbali na kuridhia, Pambazuko lilimtaka Rais Samia kuunda Kurugenzi ya Kuchunguza Polisi, ambayo itafanya kazi chini ya ofisi yake, Ikulu.

Ifahamike kuwa sifa za utendaji wa Jeshi la Polisi Tanzania zimekuwa zikibadilikabadilika kila mara kutegemea nani ni mkuu wa nchi na zaidi sana, nani ni Inspekta Jenerali (IGP) kwa wakati huo.

Hakuna siri hata kidogo kwamba kila IGP anakuwa na zama zake; wapo waliofanya kazi vizuri – bila kujiingiza kwenye mtungo wa majambazi, wauza dawa za kulevya, majangili, wanyang'anyi, mafisadi, na sasa watekaji na wauaji.

Lakini pia wapo wakuu wa jeshi letu la Polisi walioamua kujiunga na magenge ya hovyo kwa ajili ya kupata utajiri haramu wa harakaharaka.

Hawa wakuu wa kundi la pili ndio walioharibu kabisa nidhamu na sifa ya jeshi hilo lenye majukumu makubwa ya kulinda watu na mali zao. Hawa walishiriki kuteka, kutesa na hata kuua, kubambika kesi na kuamuru wasaidizi wao kupora mali halali za wananchi, ilimradi wao wapate mali kwa kuumiza wengine.

Ni hawa wa kundi la pili ndiyo walikuwa wakijiona mungu-watu, kiasi kwamba hawakuwa hata na chembe ya kumuogopa Amiri Jeshi Mkuu kwa sababu ambazo wanazijua wao wenyewe.

Taarifa kwamba watuhumiwa wamepokwa mali zao, kuteswa na hata baadhi ya watuhumiwa kufia mikononi mwa watendaji wa jeshi hilo, zimekuwa "za kawaida sana."

Kunapotokea matukio haya ya hovyo, ni watendaji wa jeshi hilohilo ndiyo hupangwa kuchunguza kilichotokea, hatua ambayo, kwa mizania yoyote ile haiwezi kuwa ya haki hata kidogo.

Hivi inawezekanaje mtuhumiwa akachunguzwa na watuhumiwa wenzake? Kwamba linalotuhumiwa ni jeshi, na wachunguzi wanakuwa wao. Hapa hakuna haki inayoweza kutendeka, isipokuwa kufichwa kwa ukweli na watuhumiwa kuachwa huru, hata kama kuna kila dalili kwamba walitenda uovu.

Ni kutokana na sababu hizo na kuongezeka kwa tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, sisi katika Pambazuko tunaona wakati umefika sasa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kuunda Kurugunzi Huru ya Upelelezi kwa Polisi.

Tunapendekeza kwamba ikiwa Rais ataridhia kuundwa kwa kurugenzi hiyo, iwe ni sehemu ya watendaji walioko ofisini kwake – Ikulu, ili kuwepo na ufanisi na kuleta matokeo yanayotarajiwa kwa kila uchunguzi unaofanywa dhidi ya Polisi na watendaji wake.



Karibu Balozi Mshana...



Balozi wa Tanzania nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Said Juma Mshana (kushoto) amekutana na Waziri Mkuu wa DRC, Judith Simunwa Tuluka jijini Kinshasa hivi karibuni. Katika kikao hicho, Balozi Mshana aliwasilisha salamu za pongezi kwa Waziri Mkuu kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa nchi hiyo, Felix Antoine Tshisekedi. (Picha na Balozi)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon **MKINA**	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter **NYANJE**	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi **PAUL**	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth **HOMBO**	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew **MSECHU**	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin **LUPATU**	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia **MFINANGA**	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Habari

Sifa za anayefaa kuongoza Tanzania



Viongozi mbalimbali walioshiriki Uzinduzi wa Ilani ya uchaguzi ya AZAKI iliyopewa jina la "TANZANIA TUITAKAYO", iliyozinduliwa jijini Arusha Septemba 12,2024. (Na Mpigapicha Maalum)

Na Elizabeth HOMBO

ASASI za Kiraia (Azaki) nchini zimetoa msimamo kuhusu misingi mikuu ya kuongoza nchi ambayo wangependa kuona Tanzania inakuwa nayo katika kipindi kuelekea mwaka 2050.

Aidha, Azaki zimeainisha sifa kumi ambazo mtu anayefaa kuingoza Tanzania anatakiwa kuwa nazo, wakati huu ambapo nchi inajiandaa kwa Uchaguzi Mkuu mwaka kesho, 2025.

Msimamo huo umetolewa kupitia Ilani ya Uchaguzi ambayo imeandaliwa na Azaki, ambayo inaainisha misingi ya kiuongozi na sifa za viongozi binafsi kama dira kuu ya kuifikisha nchi kule ambako kila Mtanzania atakuwa na ustawi.

Aidha, katika ilani hiyo Azaki zimeainisha vipaumbele saba ambavyo vinapaswa kutekelezwa ili kuipata Tanzania yenye neema kwa watu wote.

Ilani hiyo imezinduliwa wiki iliyopita, ikiwa imebaki miezi miwili kufanyika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na takribani mwaka mmoja kabla ya kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu mwakani.

Lengo la ilani hiyo ni kutoa vipaumbele ambavyo vinapaswa kuzingatiwa na vyama mbalimbali vya siasa ambavyo vitasimamisha wagombea katika uchaguzi ujao.

Ilani hiyo inalenga kuhakikisha kuwa uchaguzi unakuwa huru na haki, huku asasi hizo zikivisihi vyama vya siasa kuzingatia yaliyomo katika ilani hiyo watakapokuwa wanaandaa ilani zao za uchaguzi.

Ilani hiyo iliwasilishwa kwa niaba ya asasi hizo na Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, jijini Arusha juzi – Jumamosi, ambako ilifanyika hafla ya uzinduzi wake.

Jopo la viongozi wa vyama vya siasa, akiwemo Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema pamoja na Katibu wa Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa wa CCM, Rabia Abdallah.

Aidha, viongozi wengine wa vyama walioshiriki kuizindua Ilani hiyo ni Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Hamad Msoud, Askofu Nelson Kisare ambaye ni mwenyekiti wa asasi ya Interfaith, Deus Kibamba aliyewakilisha vyama visivyo vya kiserikali (CSOs), Maalim Hassan Juma kutoka Angoza na Jane Magigita akiwakilisha makundi ya wanawake.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Olengurumwa alisema ilani hiyo imetaja baadhi ya sifa anazopaswa kuwa nazo kiongozi anataka kuiongoza Tanzania.

Ilani imeanisha kuwa baadhi ya sifa anazopaswa kuwa nazo mtu anayepaswa kuingoza Tanzania ni lazima awe mtu mtetezi na mlinzi wa katiba na haki za binadamu kuanzia ngazi za chini za serikali hadi ngazi za juu.

Sifa nyingine ni mtu ambaye yuko tayari kuleta taifa pamoja, kujenga Tanzania upya, kueneza mshikamano na kuhamasisha umoja wa kitaifa uliojengeka kwa misingi ya kikatiba.

Inaendelea Uk. 26

Jicho la Tai

Rambirambi kuu ni kupatikana wauaji wa Kibao

Na Igo Al

MTANZANIA mwenye asili ya Kihabeshi, anayeishi Mtaa wa Mpakani A, Kijitonyama, Dar es Salaam, akiitwa Mzee Tai, leo ameamka vibaya! Ni kama amechefukwa. Kuna jambo limemtinga kichwani mwake.

Hataki kuzungumza na mtu. Hata mkewe anaonekana kumkera, kwani alipomsabahi, hakuitika salamu yake.

Tangu asubuhi amekunja ndita. Uso wake unaonekana mzito, ingawa aliswaki na kusafisha uso kwa maji ya moto, kama kawaida yake.

Hakupokea pia salamu za shikamoo kutoka kwa mtoto wake, na hata rafiki yake kipenzi, mjukuu wake wa kwanza, naye alikiona "cha mtema kuni" – baada ya kujipendekeza kumkumbatia.

Mjukuu "alikutana na keleb" ambayo hataisahau. Alipigwa kwenzi na kuangua kilio ambacho kilimpa hasira bibi yake na ndipo Mzee Tai akafungua kinywa.

"Hivi sasa wewe mzee unazeeka vibaya, kwanini unampiga mjukuu namna hiyo, hujui kuwa umemuumiza, tena bado mdogo, ukoje wewe, leo umepatwa nini?

Mzee Tai akafungua kinywa chake na kujibu; "leo naomba mniache kabisa, kichwa changu hakiko sawa, hivi nyie mnadhani ni jambo dogo kupoteza rafiki yako mliyeshibana miaka mingi, tangu mkiwa vijana..."

"Tena amekutwa amekufa baada ya mwili wake kutupwa na hao, wewe na wenzako, mnawaita watu wasiojulikana, wakati wanawajua..."

"Yaani wewe huna habari kwamba Kibao, yule rafiki yangu tuliyekuwa naye jeshini na baadaye kustaafu pamoja, walimteka, wakamtesa na sasa wamemuua na kuutupa mwili wake huko Ununio..."

"Hivi mnadhani ni jambo dogo hilo, binadamu, tena mtu mzima, aliyekuwa anakaribia kumaliza siku zake hapa duniani, mnamteka na kumuua kwa ukatili namna ile, yaani sina raha kabisa..."

"Halafu nasikia watu wako kutoka kwa serikali yako eti wamepeleka ubani na rambirambi kwa familia ya rafiki yangu Kibao, bila aibu wanapeleka fedha, dhahabu na manemane..."

"Hivi lini mtakua nyie? Familia ya Kibao kwa sasa haitaki hizo mali, yenyewe inataka kupatiwa majina na sura za wauaji wa mume, baba, babu, mjomba na mkwe wao..."

"Hebu waambie huko wenzako wapeleke wauaji na umma wa Watanzania na hata dunia, iwatambue na wafikishwe mbele ya vyombo vya sheria na wanyongwe haraka. Kwanini hamkui? Alimaliza hasira zake Mzee Tai na kwenda kunywa kahawa hapo jirani.

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263 .

Habari Kuu

Mapya, magumu mauaji ya Kibao



Kipande cha zuria la plastiki kilichokuwa kimefunika sehemu ya mwili wa aliyekuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Chadema, Mohammed Ali Kibao. Kipande hicho hadi jana kilikuwa eneo la tukio. (Picha na Fidelis Felix)

Na Waandishi WETU

ASUBUHI ya Jumamosi Septemba 7 mwaka huu haikuwa nyepesi kwa baadhi ya wakazi wa eneo la Block F, Mtaa wa Ununio, Kinondoni, Dar es Salaam, baada ya kushuhudia mwili wa binadamu umetupwa pembezoni mwa barabara.

Mwili huo ulionwa na mpita njia majira ya saa 11:45 alfajiri ambaye aliamua kuendelea na safari yake, lakini baadaye nafsi ikamsuta na kuamua kurejea eneo lile ili kuona namna ya kutoa taarifa kwa viongozi wa eneo hilo.

Wakati anarejea, ikiwa zimepita dakika kama 15 hadi 20, alikuta kuna idadi ndogo ya watu wamekusanyika pembezoni mwa Barabara ya Ununio, wakijadili namna ya kusambaza taarifa za kupatikana kwa mwili huo.

Muda huo tayari ilikuwa kumekucha na idadi ya watu ikiongezeka eneo hilo, wakiwamo majirani ambao walitambua mwili huo kuwa ni wa mtu wa makamo, mwenye rangi nyeupe – karibu sawa na asili ya Kiarabu.

Pambazuko limeelezwa na mashuhuda kwamba mwili huo uliokuwa umelala kifudifudi, uso ukiangalia ardhini – kukiwa na nyasi chache, ukiwa umefunikwa kwa kipande cha zulia la plastiki kuanzia kichwani hadi mgongoni.

Mwili huo ulikuwa umevalishwa shati mkono mmoja wa kushoto, na suruali ikiwa imeshushwa hadi mapajani na miguu ikiwa imebaki ndani ya soksi baada ya viatu kuvuliwa na kuwekwa kando. Viatu vilivyokutwa pembeni ni rangi nyeusi.

Mashuhuda walishtushwa zaidi baada ya askari polisi kutoka Kituo cha Mbweni kufika majira ya saa moja asubuhi na kuugeuza mwili huo kuulaza chali; uso ukiangalia angani, ambapo uso huo ulikuwa hautambuliki kutokana na kutapakaa damu, huku macho yote mawili yakiwa yametobolewa.

Taharuki ya wakazi na wapiti njia hao ilikuwa ni mwendelezo wa taharuki iliyowapata ndugu, jamaa, marafiki na maswahiba wa mtu aliyekuja kutambulika baadaye kuwa ni Mohammed Ali Kibao, ambaye saa chache kabla, jioni ya Ijumaa Septemba 6, mwaka huu zilisambaa taarifa za kutekwa kwake.

Hawa, bila kujijua walijikuta wakiungana na familia na Watanzania ambao tayari walikuwa katika taharuki baada ya kusambaa kwa taarifa kuhusu namna Kibao alivyotekwa na watekaji kutokomea naye kusikojulikana.

Ilielezwa kuwa watu wasiojulikana wakiwa na silaha za kivita walizuia basi la Tashrif lililokuwa likielekea Tanga kwenye eneo la Tegeta Kibo, ambalo Kibao alipanda kutoka kituo cha Shekilango, kisha kuingia na kumchukua kwa maelezo kwamba wao ni polisi na kwamba “wana shida naye.”

Pambazuko ambalo linaendelea kufuatilia kwa karibu mtiririko wa matukio hadi kutekwa, kuuawa na mwili wa Kibao kukutwa ukiwa umetupwa kwenye eneo la Ununio.

Mwili wa Kibao ulitupwa eneo la wazi, kando tu ya barabara na siyo eneo la karibu zaidi lenye msitu wa mikoko, ambalo huenda wengi wangetarajia ili kuficha mwili huo usionekane kwa wakati.

Inaendelea Uk. 7

Habari Kuu

Mapya, magumu mauaji ya Kibao

Inatoka Uk. 6

Swali la kujiuliza, je wauaji hao walipatwa na mshtuko baada ya mateso kwa muathirika wao kuzidi kipimo na kuhisi labda hajafa amezimia tu, hivyo kumtekeleza eneo hilo wakiwa wameemvua viatu na shati ili kwamba huenda akipigwa upepo wenye baridi baada ya muda anaweza kuzinduka?

Uchunguzi wa gazeti

Pambazuko lilifika kwenye eneo la tukio, muda mfupi baada ya Jeshi la Polisi kuondosha mwili wa Kibao, ikiwa ni saa 2:51 asubuhi ambapo lilishuhudia kuwepo kwa mabaki ya damu mbichi.

Mabaki hayo ya damu yanaashiria kuwa mwili wa Kibao ulitupwa hapo saa tano kabla ya Pambazuko kufika, hivyo ikiwa ni muda huo, basi uhakika ni kuwa mwili huo ulitupwa kati ya saa 9:30 hadi 10:51 alfajiri.

Dhana hiyo ya uchunguzi wa damu kwa macho, inabebwa na uthibitisho wa kisayansi kuwa damu ikiwa kidogo zaidi, hukauka kati ya dakika 1- 3, kwenye mazingira ya joto.

Lakini katika mazingira ya baridi, damu hiyo inaweza kuchukua dakika kati ya 10-30, ingawa muda huu wote, hutegemea pia wingi wa damu.

Damu ya Kibao, ambayo haikuwa nyingi sana eneo alipotupwa – kwa vigezo vya kitaalamu, ingeweza kukauka baada ya saa 6:30 hadi 8, hasa wakati ambapo jua "lingeshika kasi" kuanzia saa 2:15 asubuhi.

Utaalamu wa kuchunguza matukio ya mauaji – hasa ya kumwaga damu, ambao Pambazuko linao, unaonyesha kuwa damu ya binadamu, ikitoka kwenye mwili, kwa sababu zozote zile, hukauka mapema zaidi inapokutana na nyuzi joto kuanzia centgrade 20.



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Ununio, Mwinyijuma Shehe, akizungumza katika mahojiano na waandishi wa habari wa gazeti hili ofisini kwake, Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na Fidelis Felix).

Kauli ya binti wa marehemu

Akizungumza na Pambazuko kwa niaba ya familia, binti wa Kibao, Miriam alisema wana maumivu ya kifo cha ghafla kisichotarajiwa cha baba yao, ambacho bado kimebaki kuwa kitendawili kinachohitaji kuteguliwa.

Alisema katika mazungumzo yake na Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, ambaye alirudi nyumbani kwao baada ya kutoka makaburini walipomzika baba yao, aliwasilisha maoni yake kwake, ikiwa ni moja ya mahitaji ya familia kwamba wahusika wapatikane na haki ionekane imetendeka.

"Nakumbuka kwenye mazungumzo yangu na waziri hapa nje, aliporudi baada ya kumaliza kumzika baba kule makaburini, hilo ni jambo ambalo nililizungumzia kwamba sisi wanafamilia tuna haki ya kupata ufumbuzi wa hili kwa sababu hatujui ni nani na wala hakuna mtu ambaye tuna mashaka naye au kumdhania..."

"Tunataka kujua muhusika wa hili jambo ni nani kama njia pekee ya kusaidia kupunguza

Inaendelea Uk. 8



Habari Kuu

Mapya, magumu mauaji ya Kibao

Inatoka Uk. 7

maumivu ya familia, suala la msingi ni kwamba hatuwezi kurudisha uhai wa mzee wetu, ila angalau haki ipatikane, hilo linaweza kupooza machozi yetu...”

“Tunaomba hiyo, kwa maana tunaamini pengine kupatikana kwa ufumbuzi wa hili, ikawa ndiyo mwisho wa matukio ya aina hii, hilo ndilo tunalohitaji kwa sasa, kuona likifanyika kwa haraka na si vinginevyo,” alisema Mariam.

Simulizi ya walioshuhudia

Akizungumza na Pambazuko katika mahojiano maalumu ofisini kwake, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Ununio, Mwinjuma Mwinyihija Shehe amesema ni wazi kwamba tukio la mwili wa Kibao kutupwa eneo hilo lilifanyika usiku wa Ijumaa Septemba 6, 2024 kuamkia Jumamosi Septemba 7, 2024.

“Siku hiyo ambayo mwili huo ulikutwa ukiwa umetelekezwa hapo ilikuwa ni Jumamosi ambayo kimsingi siyo siku ya kazi, kwa hiyo mimi niliamka mapema saa 11 alfajiri na kutoka hapa kwenda Chanika kwa shughuli zangu binafsi.



Mkazi wa Ununio aliyeshuhudia mwili wa aliyekuwa Mjumbe wa Sekretarieti ya Chadema, Mohammed Ali Kibao akionyesha kipande cha zuria la plastiki kilichokuwa kimefunika sehemu ya mwili aliyodai ulikuwa umeharibiwa vibaya. (Picha na Fidelis Felix).

“Nikiwa mwenge majira ya saa 12 asubuhi kuna mwananchi alinipigia simu akiniuliza niko wapi, nikamweleza niko njiani kuelekea Chanika. Aliniuliza una taarifa za kilichotokea huku, nikamwabia hapana.

“Mwananchi huyo alinieleza kuwa yuko eneo la Ununio Block F, karibu na kwa Wasomali, wamekuta mwili wa mtu wasiyemjua mwenye asili ya Kiarabu, nikamuuliza kuwa ni mtu wa eneo letu, anamfahamu, akasema hapana, inaonekana kuwa ni mwili wa mtu mgeni kwenye eneo hili...”

“Nilichukua hatua ya kuwapigia Polisi Jamii, kwa kijana wangu kamanda Shaban Yasin, ambaye alipokea taarifa hiyo na kwenda kuangalia eneo la tukio, tukio lilivyo ili naye atoe taarifa Polisi.

“Alipofika kwenye eneo la tukio, alinieleza kuwa alikuta tayari polisi wameshafika, hivyo aliwaambia kama wameshafika basi waache waendelee kufanya kazi yao,” alisema Shehe.

Alieleza kuwa baada ya mrejesho huo aliendelea na safari yake na alirejea usiku, siku ya pili, yaani Jumapili ndipo akasikia taarifa kuwa mtu ambaye mwili wake ulitupwa eneo hili alikuwa kada wa Chadema.

Mwenyekiti huyo wa Mtaa wa Ununio alisema eneo hilo limekuwa sehemu hatari na mara kadhaa miili ya watu waliouawa imekuwa ikiokotwa hapo.

Siku za hivi karibuni kiliokotwa kichwa cha mwanamke, huku sehemu nyingine za mwili huo ziliokotwa maeneo mengine ya jirani. Eneo hilo limekuwa likitumika kutupwa hata miili ya vitoto vichanga.

Alisema bahati mbaya zaidi upande mmoja wa barabara katika eneo hilo hatarishi, kuna maeneo ya watu ambayo pia hayajaendelezwa na yanakaa walinzi, ikifika jioni ni kiza totoro, hakuna hata taa za barabarani.

“Eneo hili limekuwa likihusishwa na ubakaji na hata wanawake kutoka maeneo mengine wamekuwa wakiokotwa wakiwa wamefanyiwa mambo mabaya baada ya kuleweshwa, kisha kutupwa hapo, limekuwa ni eneo ambalo ni kawaida kukuta lolote baya wakati wowote,” alisema.

Inaendelea Uk. 27

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Kifo cha Kibao 'kuanika' weledi wa Jeshi la Polisi

WIKI iliyopita, Tanzania ilishuhudia tukio la kusikitisha lililoibua maswali mengi kuhusu usalama wa viongozi wa upinzani nchini.

Mohammed Ali Kibao, kiongozi mwandamizi wa chama cha upinzani cha Chadema, alipotea kwa siku moja kabla ya maiti yake kupatikana katika hali ya kutisha.

Maiti ya Kibao iligunduliwa ikiwa imemwagiwa tindikali, jambo lililoashiria ukatili mkubwa na kusababisha mshtuko kwa jamii ya Tanzania na jumuia ya kimataifa.

Tukio hili liliibua wasiwasi mkubwa kuhusu hali ya kisiasa na usalama wa wanasiasa wa upinzani nchini Tanzania.

Kupotea na kifo cha Kibao kumeibua maswali mengi kuhusu uhuru wa kisiasa na haki za binadamu katika nchi yetu.

Viongozi wa upinzani na wanaharakati wa haki za binadamu na hata waandishi wa habari, wametoa mwito kwa serikali kufanya uchunguzi wa kina na wa haki.

Kufuatia tukio hili la kutisha, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, alitoa madai mazito kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mbowe alitaka hatua za haraka zichukuliwe ili kuhakikisha uchunguzi wa kina unafanyika na wahusika wanapatikana.

Madai yake yalijumuisha mambo yafuatayo, kwanza kuleta wachunguzi kutoka Scotland Yard, shirika la upelelezi la Uingereza linalojulikana kimataifa kwa weledi wake.

Pia, kuwafuta kazi viongozi wakuu wa vyombo vya usalama.

Na pengine kutoa muda wa mwisho wa Septemba 21, 2024, kwa serikali kutekeleza madai hayo.

Mbowe alitoa onyo kwamba endapo madai hayo hayatatekelezwa kufikia tarehe 21 Septemba, Chadema itaanza maandamano makubwa katika Jiji la Dar es Salaam kuanzia Septemba 23.

Tishio hili la maandamano linaonyesha uzito wa suala hili na msimamo thabiti wa chama cha upinzani katika kutafuta haki kwa kifo cha Kibao.



Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime.

Tayari Jeshi la Polisi limeyapiga marufuku maandamano hayo, huku Chadema wakisisitiza kuwa wataandamana.

Tayari kumeibuka mjadala mkubwa kuhusu uhuru wa kisiasa, usalama wa viongozi wa upinzani, na umuhimu wa kuhakikisha haki inatendeka.

Jamii ya kimataifa pia inafuatilia kwa karibu maendeleo ya suala hili, huku shinikizo likiendelea kuongezeka kwa serikali kuchukua hatua za haraka na za uwazi.

Hatua zinazochukuliwa na serikali katika siku zijazo zitakuwa na umuhimu mkubwa katika kuamua mwelekeo wa siasa na demokrasia nchini Tanzania.

Wananchi wengi wanasubiri kwa hamu kuona jinsi serikali itakavyoshughulikia suala hili nyeti na ikiwa haki itatendeka kwa familia ya marehemu Kibao na chama cha Chadema kwa ujumla.

https://instagram.com/evarist_chahali

Tafakuri ya Bagonza

Mwanga wa Mwanga umezimika ghafla

Na Dkt. Benson BAGONZA

ASKOFU Chedy Sendoro, umeniacha porini. Ulikuwa Mwanga wa wana Dayosisi ya Mwanga. Ulikuwa chachu ya wana Utatu : Karagwe, Mwanga na Pare. Kuondoka kwako kunafifisha mwanga wa wana Utatu.

Wewe ni mwana KKKT. Mzaliwa wa kwanza wa Dayosisi namba 25: Mwanga. Kiungo halisi katika nyumba ya Maaskofu. Kipenzi cha kila Askofu. Kumchukia yeye ni kujichukia.

Umeacha alama kote katika Mwanga, KKKT, CCT, na katika Utatu wetu. Ulikuwa na deko kwa sababu una wazazi, ulipendeka kwa sababu hukuwalazimisha waliokupenda.

Ulikuwa na nafasi ya pekee kwangu; uliweza kuniambia nisiyoweza kuambiwa na wengine. Uliponyamaza tulihisi unaharibu kitu.

Ulipofurahi tulijua kuna jambo laja. Ulijaliwa kusema ukweli bila kuudhi kama wengine tulivyo.

Ulipendwa na wanaokujua na wasiokujua. Ama kweli Mungu anajua kuvuna kilicho bora na kutubakiza magarasha.

Wapo ambao wakiondoka pengo lao linazibika. Lako tutaliziba lakini kivuli chako kitatutesa. Oh! Nimeomboleza vibaya.

Mungu alikupa kila kitu akakunyima uzee. Nitakuzika japo nilitamani unizike.

Tuonane utakaponiona.

Karagwe inaomboleza bila mfariji wa duniani. Kwa hakika Mwanga wa Mwanga umezimika kama mshumaa.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.





Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Haikubaliki wagonjwa kufa kwa uzembe



Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka

TUKIO la mama mjamzito kufariki dunia kwa kuchelewa kusafirishwa kutoka Kituo cha Afya Kidodi, wilayani Kilosa, Morogoro na kwenda Hospitali ya Mtakatifu Kizito, Mji Mdogo wa Mikumi, eti kwa ukosefu wa mafuta na dereva kwenye gari la wagonjwa, haliwezi kupita bila ya kujadiliwa.

Kwa mujibu wa taarifa zilizochapishwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari, tukio hilo limetokea wiki iliyopita na kumsukuma Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka kukimbia upesi kwenye eneo hilo na kufanya mkutano wa dharura ili kusikiliza kero hiyo.

Shaka katika mkutano huo alipata nafasi ya kusikiliza kilio cha wananchi wa Kidodi wanavyolalamikia kutozwa shilingi 180,000 ikiwa ni mchango wa mafuta kwa gari la wagonjwa la serikali kwa mama mjamzito aliyepewa rufaa kwenda Mikumi!

Akihitimisha mkutano huo Shaka aliwaomba wananchi kuwa watulivu kipindi hiki ambacho serikali ya wilaya imeunda tume kuchunguza tukio hilo na kuahidi kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote atakayebainika kuhusika na kifo cha mwana mama huyo.

Matukio kama haya yanayohusisha kucheleweshewa huduma muhimu hadi kusababisha kifo cha mama mjamzito, ni uthibitisho kuwepo hali mbaya ya utoaji wa huduma za afya nchini Tanzania.

Katika mwaka wa 2017, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mbeya alifariki baada ya kucheleweshwa kupatiwa huduma ya dharura kutokana na ukosefu wa mafuta ya gari la wagonjwa.

Mwanafunzi huyo alikuwa na hali mbaya ya afya na alihitaji usafiri wa haraka hadi hospitali, lakini huduma hiyo ilichelewa kwa sababu ya ukosefu wa mafuta.

Mwaka 2019, mjane aliye na hali mbaya ya afya alifariki baada ya kucheleweshwa kwa saa kadhaa kupata usafiri wa gari la wagonjwa.

Kituo cha afya kilichelewa kutoa huduma kutokana na ukosefu wa fedha za mafuta na ukosefu wa madereva wa gari la wagonjwa.

Kiukweli changamoto kubwa katika sekta ya afya ni ukosefu wa rasilimali, ikiwemo mafuta kwa magari ya wagonjwa na fedha za dharura.

Hali hii inaathiri moja kwa moja uwezo wa vituo vya afya kutoa huduma za haraka kwa wagonjwa.


Uzembe wa watoa huduma za afya nao unajitokeza wazi katika matukio haya. Kuchelewa kwa usafiri wa wagonjwa kwa sababu ya kutokuwa na mafuta au fedha za mafuta, ni uzembe wa wazi na haukubaliki.

Hoja yangu ni serikali inapaswa kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za dharura kwa kuhakikisha kuwa vituo vya afya vinapata fedha za kutosha kwa ajili ya mafuta na huduma za dharura.

Aidha mikakati ya dharura inapaswa kuwekwa ili kuhakikisha kuwa gari la wagonjwa linakuwa na mafuta kila wakati.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Kurunzi la Intelijensia



Na Godwin CHILEWA,
Houston

Hili la utekaji liamshe serikali kuchukua hatua



Vitendo vya utekaji

KATIKA miezi ya hivi karibuni, nchi yetu imekumbwa na ongezeko la kutisha la utekaji nyara, ambapo raia wasio na hatia, hususan viongozi wa upinzani.

Licha ya ushahidi unaozidi kuongezeka na kelele za umma, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camillus Wambura, amekuwa akikanusha tuhuma hizi, jambo linalowaacha raia wakiwa na hisia za usaliti na wasiwasi mkubwa kuhusu usalama wao.

Serikali, na hasa Rais Samia Suluhu Hassan, lazima wachukue hatua za haraka na thabiti kushughulikia tatizo hili linalozidi kuwa kubwa.

Kadiri ripoti za utekaji nyara zinavyoendelea kusambaa, imani ya umma kwa serikali na taasisi zake inazidi kuporomoka.

Raia hawana tena imani kuwa vyombo vya usalama vinaweza kuwalinda, na ukimya wa mamlaka unaongeza tu shaka kwamba kuna mengi zaidi katika utekaji nyara huu kuliko inavyoonekana.

Kutotaka kwa Jeshi la Polisi kukiri tatizo hili na kuchukua hatua haraka, kunachochea hasira na kukata tamaa, huku wengi wakituhumu utawala kwa uzembe au, hata zaidi, kushirikiana kwa namna fulani na uhalifu huu.

Waathirika wa utekaji nyara siyo takwimu tu; ni raia wenzetu, akina mama, akina baba, wanaharakati, na viongozi wa vyama vya upinzani.

Mateso yao, katika mfumo wa unyanyasaji wa kimwili na kiakili, hayawezi kupuuzwa. Mateso na kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria, ni uvunjaji wa haki za binadamu na utawala wa sheria, misingi muhimu ya jamii yoyote ya kidemokrasia.

Kwa kila mwathirika, kuna familia iliyobaki ikihuzunika, jamii inayoishi kwa hofu, na taifa lililoko kwenye njia panda ya kutumbukia kwenye vurugu.

Ili kushughulikia tatizo hili, serikali kwanza inapaswa kutambua uzito wa hali hii na kisha kuchukua hatua za haraka kuwakamata waliohusika.

Hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na serikali inapaswa kuunda tume huru kufanya uchunguzi wa kina juu ya madai ya utekaji nyara na mateso.

Tume hii lazima ijumuishwe na wawakilishi kutoka asasi za kiraia, mashirika ya haki za binadamu, na wataalam wa sheria ili kuhakikisha usawa.

Ushiriki wa vyombo huru utasaidia kurejesha imani ya umma katika mchakato huo na kuhakikisha kuwa haki inatendeka na kuonekana inatendeka.

Pia askari polisi au watu binafsi watakaopatikana kuhusika na utekaji nyara huu, lazima wafikishwe mbele ya sheria. Mfumo wa sheria lazima uendeshwe bila kuingiliwa, wala upendeleo kwa wale walio madarakani.

Kuwachukulia hatua wahalifu kutatoa ujumbe mzito kwamba hakuna aliye juu ya sheria, na serikali haitavumilia uvunjaji wa haki za binadamu kwa namna yoyote ile.

Aidha, ni wakati muafaka sasa kurekebisha Jeshi la Polisi, hasa mabadiliko ya kimuundo yanahitajika haraka ili kukabiliana na rushwa, ukosefu wa uwajibikaji, na matumizi mabaya ya madaraka ndani ya jeshi hilo.

Itaendelea wiki Ijayo...

Mwandishi ni mchambuzi wa masuala ya intelijensia, na mwandishi wa vitabu. Anaishi Houston, Texas, Marekani.



Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

Buriani Askofu Chediel Elinaza Sendoro



Askofu Chediel Elinaza Sendoro

SEPTEMBA 9, 2024 ilikuwa siku ya simanzi kuu kwa jamii ya wengi hapa nchini na hata nje ya nchi, baada ya kupokea taarifa za kushtua kuwa Askofu Chediel Elinaza Sendoro wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mwanga, amefariki dunia kwa ajali ya gari iliyotokea katika eneo la Kisangiro wilayani Mwanga, Kilimanjaro.

Askofu aliyefariki ni mmoja kati ya maaskofu 27 wa KKKT na ni mmoja wa maaskofu vijana wa kanisa hilo. Huyu ndiye alikuwa askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Mwanga ambayo ilipatikana baada ya mgogoro mgumu uliokuwa umeikumba Dayosisi ya Pare.

Nimemsoma Askofu Benson Bagonza wa Dayosisi ya Karagwe, akiomboleza kwa uchungu kifo cha Askofu Chediel na ninaungana naye kuwa mwanga wa Mwanga umezimika kama mshumaa.

Kwa nini tunasema alikuwa mwanga wa Dayosisi ya Mwanga? Itakumbukwa kuwa akiwa kijana mdogo alipokea jukumu kubwa sana la kuiongoza dayosisi hiyo mpya kabisa ambayo ilihitaji umakini mkubwa sana kutokana na muktadha wa uanzishwaji wake.

Kwa umahiri mkubwa, alilibeba jukumu hilo na akafanya vitu vilivyoonekana vya kuunganisha wana dayosisi na hata na dayosisi iliyokuwa dayosisi mama yaani Dayosisi ya Pare.

Kwa kiasi kikubwa amefanikiwa kujenga umoja kati ya watu katika dayosisi na kati ya dayosisi na dayosisi.

Binafsi nimemfahamu Askofu Chediel tangu akiwa mwanafunzi, wakati wazazi wake wakiwa wanatumika katika Usharika wa Kurasini.

Niliendelea kufahamiana naye hadi baba yake akawa Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Masharki na Pwani ya KKKT, Baba Askofu Eilinaza Sendoro ambaye kwa sasa ni mstaafu.

Haiba aliyokuwa nayo Askofu Chediel inaonekana wazi kurithishwa kutoka kwa baba yake kwani alikuwa na upendo, upole, ucheshi, unyenyekevu na hata hali ya kutobagua.

Askofu huyu kijana amezaliwa mwaka 1970 akiwa ni mtoto wa nne wa Baba Askofu Elinaza Sendoro na Mama Joyce Sendoro, kwa umri huu wa miaka 54 unasababisha watu kutamani angeendelea kuwepo, kwani ni umri wa kutumika, umri wa nguvu, mategemeo na tumaini.

Tulimuona alipofanya kazi akiwa katika Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Shirika la Evangelical United Mission (EUM) na alikuwa kiongozi wa kundi la maombi lijulikanalo kama PATMO.

Tunapompa Buriani Askofu Chediel tunatoa pole nyingi kwa wazazi wake; Askofu na Mama Askofu Elinaza Sendoro, mke wake, Marystella Sendoro na watoto wake; Eric na Erica pamoja na wana Dayosisi ya Mwanga na kanisa zima la KKKT kwa kuzimika ghafla kwa mpendwa wao.

Mungu aipumzishe roho ya Askofu Chediel Sendoro mahali pema peponi.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

Habari

Wanasubiri nini kujiuzulu?

Na Waandishi WETU

KUTEKWA, kuteswa na hatimaye kuuawa kwa Mkuu wa Usalama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mohammed Ali Kibao, kumeibua shinikizo la kutaka wenye dhamana ya vyombo vya ulinzi na usalama, kuwajibika.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camillus Mongoso Wambura ndio hasa wanakamiwa, wakitakiwa kujiuzulu kwa njia ya "kuwajibika."

Wanaotoa shinikizo ni pamoja na viongozi wa dini, wanazuoni, wanasiasa, wanaharakati na wananchi waliokerwa na mwendelezo wa matukio ya Watanzania kutekwa, kuteswa, kutupwa wakiwa hai na, au kuuawa.

Taarifa za kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa Watanzania, zimekuwa zikionyesha kuwepo ongezeko la matukio haya, lakini kubwa zaidi, na lenye kuogofya ni lile lililomkuta Mohammed Ali Kibao, aliyetekwa Septemba 6; na kuuawa ndani ya saa 14.

Hadi sasa wauaji hawajapatikana, na serikali inaendelea kueleza kuwa "ni watu wasiojulikana;" na kwamba inaendelea kuwatafuta.

Waliomuua kada huyo wa Chadema ni watu waliojitambulisha kuwa ni polisi – wakiwa na bunduki za kivita; Sub Machine Gun (SMG) na pingu. Hii ilikuwa baada ya kuvamia basi la Tashrif alimokuwa akisafiri, pale lilipofika eneo la Kibo Commercial Centre, Tegeta, Dar es Salaam.

Muda mfupi baada ya taarifa za kifo cha Kibao kusambaa, Jumapili Septemba 8, 2024, Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza uchunguzi wa kina na wa haraka juu ya tukio hilo.

"Nimeagiza vyombo vya uchunguzi kunileta haraka taarifa ya kina kuhusu tukio hili baya kabisa na mengine ya namna hii. Nchi yetu ni ya kidemokrasia na kila raia ana haki ya kuishi. Serikali ninayoiongoza haivumilii vitendo vya kikatili vya namna hii," aliandika kwenye ukurasa wake wa X.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni

Agizo hilo lilifuatiwa na matamko kadhaa yaliyotaka Masauni na Wambura kujiuzulu nyadhifa na nafasi kwa maelezo kuwa wao ndiyo wenye dhamana ya kuhakikisha uhai wa kila Mtanzania unalindwa kwa gharama yeyote ile.

Hata hivyo, pamoja na kuongezeka kwa shinikizo kwa viongozi hao "kuachia ngazi" ili angalau kuonyesha wanajutia tukio hilo na kwamba wanathamini uhai wa kila binadamu; leo ni siku ya saba bado wako madarakani. Hawajajiuzulu.

Pambazuko limeratibu maoni ya baadhi ya Watanzania wanaoamini kuwa kujiuzulu kwa viongozi hao, kutaacha alama ya uwajibikaji na kuongeza umakini kwa taasisi zinazohusika kulinda uhai wa binadamu – kwani hauna mbadala.

Kanisa Katoliki: Wawajibike

KANISA Katoliki limevunja ukimya, ambapo limelaani na kutaka viongozi wenye dhamana kuwajibikaji baada ya "kukomaa" kwa matukio yote ya utekaji, utesaji na mauaji.

Akitoa salamu fupi za Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) kwa Kanisa na jamii ya Watanzania, Askofu Eusebius Nzigilwa wa Jimbo Katoliki Mpanda alisema jana kuwa hawaamini kwamba makundi haya ya kihalifu yana nguvu kuliko vyombo vya ulinzi na usalama.

Inaendelea Uk. 15

Habari

Wanasubiri nini kujiuzulu?

Inatoka Uk. 14

Kwamba Kanisa linaviomba vyombo vya ulinzi na usalama kutimiza majukumu yanayopaswa ili kurudisha heshima ya taifa; ya kuwa kisima cha udugu na amani.

"Pia tunatoa mwito kwa wale wote ambao hawakuwajibika kwa kadiri ya nafasi zao wawajibishwe. Uhai ni zawadi kutoka kwa Mungu, mtu ameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu mwenyewe, hivyo maisha na utu wa mtu ni lazima viheshimiwe na kulindwa kwa nguvu zote, udugu huponya ulimwengu," alisema Askofu Nzigilwa.

Alisema Kanisa linatoa pole kwa ndugu na familia za wale waliouawa, na kuwa wanawaombea marehemu wote pumziko la amani mbunguni, lakini pia alielekeza pole hizo kwa wale walioumizwa au kujeruhiwa katika matukio haya ya kihalifu.

Mwito huo ulitolewa kwenye kusanyiko la Ibada Takatifu ya Ekaristi iliyowakutanisha waumini wa Kanisa hilo kutoka majimbo yote nchini, iliyohudhiriwa na viongozi wa serikali na kutoka vyama vya siasa, akiwemo Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Biteko, Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu na Katibu wa Chadema, John Mnyika.

Askofu Nzigilwa alisema wanapoangalia Tanzania wanatambua kuwa nchi hiyo imejulikana kama kisiwa cha amani, udugu na mahali pekee Afrika ambapo raia wake, licha ya tofauti zao za kikabila, kiimani, kiitikadi na kiuchumi wameweza kuishi kwa amani na kindugu.

"Kila mtu alihakikisha anaimiliki tunu hii na kuilinda, lakini tukiangalia hali ya sasa ya nchi yetu, tunaona tunu yetu ya undugu na amani imeshambuliwa. Hii inatokana na matukio yaliyotokea nyakati za karibuni za watu kutekwa, kuumizwa na hata kuuawa.

"Najiuliza nini kimepotea kwenye tunu hii, taifa letu limekosea wapi, je, uongozi na mamlaka husika pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimezidiwa nguvu na maarifa hata kushindwa kudhibiti hali hii?" Alihoji Askofu Nzigilwa.

Katika kongamano hilo lililoongoza na kauli mbiu "Udugu Kuponya Ulimwengu" - Askofu Nzigilwa alisema watu wote wamealikwa kwenda kuishi maisha ya kiekaristi yanayojengwa katika misingi ya upendo, huruma, mapatano, msamaha na matoleo kwa ajili ya ustawi wa wote.

Mitandao yaunganisha kauli

Watumiaji wa mitandao ya kijamii, hasa Instagram, X, makundi sogozi ya WhatsApp na Facebook, wameonyesha kukerwa na kuenea kwa matukio ya kutekwa, kuteswa na hata kuuawa kwa Watazania.

Wachangiaji wa mitandao hiyo wamewataka viongozi hao wenye dhamana ya kulinda uhai wa wananchi na mali zao, kujiuzulu "haraka" ili kuonyesha kuwajibika.

Pambazuko, hadi jana, limeona zaidi ya wachangiaji 912, kutoka mtandao wa X na 237, kutoka Instagram wanaotaka Masauni na Wambura kuachia ngazi mara moja kwa kilichoelezwa kuwa ni "kushindwa kazi."

Wachangiaji hao wanaofanya jumla yao kuwa 1,149, wametaja neno "wajiuzulu" mara 1,214, hali inayowakilisha matamanio ya Watanzania wengi. Katika WhatsApp na Facebook, kuna "mafuriko" ya ujumbe wa kuwataka viongozi hao kujiuzulu.

Inaendelea Uk. 19



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Camillius Wambura

Uchaguzi Marekani





Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris

Kamala aonekana kumgaragaza Trump

Na Mwandishi WETU

KURA za maoni kutoka taasisi kubwa na wachambuzi wa masuala ya siasa za kimataifa, zimempa ushindi mgombea Urais wa Marekani kwa tiketi ya Democrat, Kamala Harris katika mdahalo alioufanya katikati ya wiki iliyopita dhidi ya mgombea wa Republican, Donald Trump.

Hata hivyo, wachambuzi wanaonya kuwa hiyo siyo dalili ya wazi ya ushindi wa urais kwa upande wa Kamala katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Novemba, mwaka huu.

Lakini ni wazi kuwa katika mdahalo huo, Kamala "alimkamata vilivyo" Trump kiasi cha rais huyo wa zamani wa Marekani kuchanganyikiwa katika hoja zake na kusababisha kurusha mashambulizi hadi kwa rais wa sasa, Joe Biden na kumlazimisha Kamala kumkumbusha:

"Unapambana na mimi, si Biden."

Jambo kubwa ambalo limemfanyaKamala kumpiku Trump ni kuwa mwanamama huyo hakukubali kuwa chini ya mfanyabiashara huyo katika masuala yaliyojadiliwa.

Tangu wanaanza mjadala huo, Kamala alihakikisha kuwa anakuwa juu katika kila jambo.

Mathalan, mara baada ya waendeshaji wa mdahalo huo kuwakaribisha, Kamala alikuwa wa kwanza kuingia na akawa na kasi zaidi na kumfikia Trump aliyekuwa "anajivutavuta" na kumpa mkono huku akijitambulisha.

Trump alijibu kwa sauti ambayo haikusikika vyema na hapo inaelekea ndipo Kamala alipoimarisha udhibiti wake dhidi ya Trump.

Hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Kamala kukutana ana kwa ana na Trump, ambaye alichaguliwa kuwa Rais wa Marekani mwaka 2016, huku Kamala akichaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Seneti.

Tangu wakati huo wamekuwa "wakipishanapishana," huku Kamala akijijengea heshima kwenye Seneti kwa maswali magumu aliyokuwa anayauliza dhidi ya maofisa wa serikali ya Trump.

Miaka minne baadaye, alishiriki katika kampeni zilizomwondoa Trump madarakani akiwa ni mgombea mwenza wa Joe Biden.

Katika kipindi chote cha dakika 90 ambazo wanasaiasa hao walikuwa jukwaani, Kamala alifanikiwa kumfanya Trump kuwa kama mtu anayejitetea kizimbani, akimbana kuhusu masuala binafsi kama vile idadi ya watu wanaohudhuria mikutano yake hadi kwenye masuala ya kisera kama vile jinsi Trump anavyogeuzageuza misimamo yake katika suala la utoaji mimba.

Bila kujijua, Trump alikuwa akiingia kwenye mitego hii ya Kamala kila mara na kujikuta akijitetea kwa muda mrefu badala ya kutoa hoja zake.

"Kwa hakika Donald Trump hana mpango wowote kuhusu ninyi (wapiga kura), hii ni kwa kwa sababu anapenda kujitetea yeye mwenyewe binafsi badala ya kuwafikiria ninyi wapiga kura," alisema Kamala, akionekana kama mwendesha mashitaka dhidi ya Trump mahakamani.

Hata wanasiasa wengine walioangalia mdahalo huo kwenye televisheni, walikiri kuwa Kamala alikuwa bora kuliko Trump.

Inaendelea Uk. 17

Kamala aonekana kumgaragaza Trump

Inatoka Uk. 16

Gavana Gavin Newsom, alimsifia Kamala akisema alionyesha umahiri wa hali ya juu.

"Alikuwa anaangalia kamera kila wakati, akizungumza kuhusu mpiga kura, kuhusu wewe, akizungumza kuhusu watu wa Marekani. Alisisitiza kuhusu masuala muhimu yanayowahusu," alisema.

"Kwa upande mwingine, mwenzake alizungumza kuhusu mbwa, idadi ya watu wanaohudhuria kwenye mikutano ya kampeni na malalamiko yake binafsi. Inasikitisha kuwa chama kimemteua mtu ambaye anatia huruma," aliongeza gavana huyo.

Kosa jingine ambalo Trump alilifanya wakati wa mdahalo ni kulazimisha kuzungumza yale anayoyataka badala ya kujibu maswali.

Anajua kuwa suala la uhamiaji limemletea umaarufu miongoni mwa Wamarekani wa ngazi za chini hivyo akawa anajitahidi kulitaja suala hilo karibu kwenye kila swali atakaloulizwa.

Hilo lilimfanya kwa ujumla aonekane hana ujumbe mahsusi na wa maana kwa wapiga kura.

Hata baadhi ya watu muhimu kwenye chama cha Republican waliona wazi kuwa mgombea wao hakufanya vizuri.

Vivek Ramaswamy, mmoja wa wanasiasa ambao walipewa nafasi ya kumrithi Trump iwapo angeondolewa kwenye kinyang'anyito hicho alisema; "tulisikia mambo mengi yakisemwa vyema na ninakubali kuwa yalitoka kwa Kamala Harris."

Lakini, Ramaswamy anaongeza kuwa kusema mtazamo wake hakumaanishi kuwa mwanamama huyo ameshinda kwani "vitendo huongea zaidi ya maneno."

Hata hivyo, haimaanishi kuwa katika mdahalo wote Trump hakuwa na muda wa kusema mambo yaliyoleta kicheko kwa waendeshaji na wasikilizaji.

Kuna wakati Trump alidai kuwa Kamala amekopi mpango wake wa uchumi na akaahidi baada ya mdahalo huo atampatia kofia yenye nembo ya Maga – Make America Great Again – alama kubwa anayoitumia kwenye kampeni zake, ikimaanisha kuirejesha Marekani kwenye enzi za ukuu wake.

Hoja mfu

Kwa ujumla, wakati Kamala akijibu maswali kwa kuelezea hoja kulingana na hali ilivyo hivi sasa katika jamii, Trump alitumia muda mwingi kurudiarudia hoja ambazo amekuwa akizirudia mara nyingi, nyingine zikiwa zimepitwa na wakati.

Alisikika kuzirudia hoja hizo kwa sababu ziliwahi kumletea umaarufu siku za nyuma.

Inaonekana Kamala atakuwa ameshinda imani ya wapiga kura ambao katika siku za hivi karibuni walieleza kupitia kura moja ya maoni kuwa wanahitaji kumfahamu mgombea huyo kwa undani.

Ni dhahiri kuwa Kamala alitumia mdahalo huo kujitambulisha kwa wapiga kura hao.

Labda kwa kuzingatia matokeo ya mdahalo uliopita dhidi ya Biden, Trump aliingia kwenye mdahalo huo pia akidhani kuwa anakutana na mtu kama Biden, lakini akakutana na kitu kingine tofauti, kwani Kamala alikuwa anajiamini, anazungumza kwa ufasaha bila kigugumizi na alijipanga kwenye hoja.

Ingawa ushindi kwenye mdahalo mara zote haumaanishi kuwa mtu anakuwa ameshinda urais, lakini kwa kilichoonekana wiki iliyopita, Trump anatakiwa afanye kazi kubwa zaidi kwenye kampeni ili kumpiku Kamala.

Mbaya zaidi, wakati Kamala akithibitisha kuwa yupo tayari kwa mdahalo mwingine, watu wa timu ya kampeni ya Trump hawajaonyesha waziwazi utayari wa kushiriki.



Donald Trump

Habari

Wakala wa Vipimo yaalika sekta binafsi



Mkurugenzi Mkuu wa WMA, Alban Kihulla

Na Mwandishi WETU

WAKALA wa Vipimo Tanzania (WMA), imewakaribisha wafanyabiashara kutoka sekta binafsi kuwekeza katika eneo hilo kwani kuna fursa nyingi ambazo hazijatumika.

Mwito huo umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa WMA, Alban Kihulla, wakati akizungumza na wahariri kuhusiana na majukumu na utendaji wa wakala huo.

"Kuna maeneo kama 17 ambayo tumeyaanisha ambayo wafanyabiashara kutoka sekta binafsi wanaweza kuwekeza katika eneo hili la vipimo nchini, kwanza kuna eneo la ukaguzi wa vipimo, ni eneo pana sana na uwezo wa wakala kulishughulikia kwa tija ni mdogo kutokana na upungufu wa watumishi," alisema.

Alisema Tanzania ni nchi kubwa na mahitaji katika sekta mbalimbali ni mengi na sekta ya umma peke yake haiwezi kutosheleza.

Hata hivyo, alisema anayehitaji kushirikiana na WMA katika shughuli zake, anapaswa kufuata taratibu kadhaa zilizowekwa na pia kuwa na vifaa vya kisasa na watu wa kutosha kwa ajili ya shughuli atakazoaminiwa kuzifanya kwa niaba ya WMA.

"Utaratibu unaratibiwa na kitengo cha sekta binafsi kilichopo Wizara ya Fedha kikiitwa PPP Centre. Ukishaenda pale utapewa utaratibu wote unaopaswa kuufuata na sisi tutaitwa kama washauri," alisema.

Aliyataja baadhi ya maeneo mengine ambayo sekta binafsi inaweza kushirikiana na WMA kuwa ni uhakikiwa mita za gesi na maji, uhakiki wa lifti na uhakiki wa mashine za michezo ya kamari.

Mkutano huo uliratibiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR) chini ya utaratibu wake wa kuwakutanisha maofisa watendaji wakuu wa taasisi za umma na wahariri ili waeleze utendaji wao.

Kihulla alitumia fursa hiyo kuwaeleza wahariri kuwa pamoja na changamoto zilizopo, lakini Wakala umefanikiwa kuimarisha utendaji na kupandisha tija.

Kwa kuonyesha kuwa WMA imekuwa ikifanya kazi nzuri, Kihulla aliwaambia wahariri hao kuwa wakala umeendelea kutoa mchango serikalini kupitia gawio.

Alisema mwaka 2019/20 , WMA ilitoa shilingi bilioni 5.3 ikiwa ni gawio serikalini huku mwaka 2020/21 ikitoa shilingi bilioni 6.2.

"Mwaka 2021/22 gawio lilipungua kidogo hadi shilingi bilioni 4.2 na hii ilitokana na janga la Covid-19 ambalo liliathiri shughuli nyingi sana, siyo tu Tanzania pekee, bali duniani kote," alisema.

Alitaja baadhi ya mafanikio ya wakala kuwa ni pamoja na WMA kushinda tuzo ya taasisi bora kati ya taasisi 258 zilizo chini ya Msajili wa Hazina kwa kuchangia gawio la serikali kwa wakati.

Aidha, alibainisha kuwa kumekuwa na ongezeko la idadi ya vipimo vilivyohakikiwa, ambapo vipimo viliongezeka kutoka 127,000 mwaka 2018 hadi 949,000 mwaka 2019. Pia Wakala huo umefanikiwa kujenga ofisi mpya za makao makuu katika eneo la Medeli jijini Dodoma.

Kihulla alieleza kuwa ujenzi wa ofisi hizio umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, mwaka huu. Ofisi hizo zinajengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 7.3.

Wanasubiri nini...



Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Deodatus Balile

Inatoka Uk. 15

Lema aonyesha njia

Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini, Gobless Lema alikuwa wa kwanza kutamka kauli wakilishi hadharani – tena usoni mwa Masauni, akishangaa kwanini bado anaendelea kushikilia wadhifa na dhamana ya waziri.

Lema, akiwa kwenye maziko ya Kibao, jijini Tanga, ambako pia Masauni alihudhuria akiwa mwakilishi wa serikali, alisema kufuatia tukio la kutekwa na kuuawa kwa Kibao na watu wanaoaminika kuwa maofisa wa vyombo vya dola, Masauni hakupaswa kuwa kiongozi hadi wakati huo na kwamba anashangaa kupata uthubutu wa kushiriki maziko hayo.

"Mheshimiwa waziri, nikuombe sana usiende tena kwenye msiba wa mtu aliyetekwa na kuuawa; nenda kwenye msiba mingine. Mnatuumiza. Nilitarajia baada ya statement (kauli)ya Rais jana, wewe leo uwe umejiuzulu; IGP amejiuzulu na viongozi wengine wakae kando.

Balile ashinikiza

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, ambaye pia ni msomi wa sheria, amemtaka Masauni kujiuzulu kama alivyofanya aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Ali Hassan Mwinyi, ambaye alijiuzulu wadhifa wake Januari 22, 1977, baada ya kutokea kwa mauaji ya vikongwe huko Shinyanga.

Mwinyi ambaye baadaye alikuja kuwa Rais wa Tanzania, aliamua kuwajibika kwa kujiuzulu na kufuatiwa na viongozi wengine waandamizi waliokuwa na dhamana ya kulinda uhai wa Watanzania.

Mwinyi alipojiuzulu, alifungua mlango wa uwajibikaji, ambako mamlaka ya uteuzi iliwastaafisha kwa maslahi ya umma, Mkuu wa Usalama wa Taifa Mkoa (RSO) Andrew Mayalla, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Peter Kisumo; Mkuu wa Usalama wa Taifa Wilaya (DSO) akiitwa Ihuya, Mkuu wa Polisi Mkoa (RPC) akiitwa Mkwawa, na Mkuu wa Polisi Wilaya (OCD). Hawa baada ya kustaafishwa walifikishwa mahakamani na baadhi wakakutwa na hatia huku wengine wakiachiwa huru.

Balile anakataa kuwa hao waliomteka na kumuua Kibao walikuwa majambazi; na anauliza kama hao walikuwa majambazi, walikuwa wanataka nini kwa Kibao – hadi kubeba SMG – labda kama angekuwa na fuko la dola za Marekani, maana majambazi mara nyingi hutafuta fedha, siyo roho za watu.

Balile anasema ili kulinda heshima yake, na kuonekana anawajibika na kuumizwa na kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa Kibao, ni vyema Masauni ajiuzulu

Mwenyekiti huyo wa TEF pia anakumbusha yaliyotokea mwaka 2013 katika kukabili ujangili; pale ilipoanzishwa Operesheni Tokomeza.

Operesheni hii ilidhibiti ujangili, lakini pia maisha ya watu yalipotea. Mawaziri wanne waliwajibika kisiasa, pamoja na kwamba hawakuwa porini kupambana na majangili.

Mawaziri waliowajibika ni aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Khamis Kagasheki; Waziri wa Ulinzi, Shamsi Vuai Nahodha; Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi; na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dkt. Mathayo David.

Balile anasema kuwa amepata fursa ya kuzungumza na baadhi ya mawaziri, baadhi ya wajumbe wa Kamati Kuu (CC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), mabalozi na wastaafu wengine, ambao wote wanabeba maoni kwamba Masauni anapaswa kujiuzulu.

Askofu Shoo atoa ya moyoni

Askofu Fredrick Shoo wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), amelaani kuendelea kuwepo kwa vitendo vya kuteka, kutesa na hata kuua raia.

Inaendelea Uk. 30

Ana kwa Ana



Mkurugenzi Mkuu mpya wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Irene Isaka (kushoto), akikaribishwa ofisini na Mkurugenzi wa Fedha wa Mfuko huo, Grace Temba. (Picha kwa hisani ya NHIF).

Isaka: Sina uvumilivu kwenye rushwa

• NHIF kuanza kutumia akili mnemba

HIVI karibuni Rais Samia Suluhu Hassan alimteua mtaalamu wa masuala ya hifadhi ya jamii, Irene Isaka, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Pambazuko lilipata fursa ya kukutana na Isaka muda mfupi baada ya kuteuliwa na kufanya naye mahojiano kuhusu masuala kadhaa.

Je, ni mabadiliko gani ambayo kiongozi huyo mwenye uzoefu mkubwa kwenye sekta ya hifadhi ya jamii amepanga kuyaleta kupitia nafasi yake hiyo mpya?

Ungana na timu ya Pambazuko katika mahojiano haya.

Pambazuko: Kwa kuzingatia uzoefu wako katika sekta ya huduma za jamii tutarajie nini kipya kutoka NHIF baada ya ujio wako?

Irene Isaka: Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu.

Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini kusimamia mfuko huu wa bima ya afya, na hasa kipindi hiki tunapoelekea kwenye utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Matarajio ya serikali ni kuona wananchi wake wote wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha ambapo njia pekee na ya uhakika, ni kila mwananchi kuwa na bima ya afya.

Inaendelea Uk. 21



Isaka: Sina uvumilivu kwenye rushwa

Inatoka Uk. 20

Mfuko ni mtekelezaji wa azma ya serikali ya kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Katika kufanikisha hili, tumejipanga kutumia zaidi mifumo ya Tehama kuwarahisishia wananchi kujiunga na kupata huduma kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya taifa ya rufaa.

Aidha, tumejipanga kutoa elimu kwa wananchi kupitia njia mbalimbali ili kumfikia kila mmoja hadi ngazi ya mtaa na kijiji.

Vilevile tutaboresha uhusiano na wadau wetu wote ikiwemo sekta binafsi na kushughulikia malalamiko yote ndani ya muda mfupi ikiwa ni pamoja na kuweka mikakati ya kuepusha malalamiko kujirudia.

Pambazuko: Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu kuondolewa kwa Toto Afya Kadi, NHIF inashughulikiaje malalamiko hayo? Kuna mipango gani ya kutoa huduma kwa makundi maalum kama walemavu, wazee na watoto?

Isaka: Utaratibu wa usajili wa Toto Afya Kadi umefanyiwa maboresho ambapo usajili kwa sasa unafanyika kwa makundi kupitia shule wanazosoma na vituo vya kulelea watoto ambapo malipo kwa kila mtoto ni Shilingi 50,400 kwa mwaka.

Aidha, watoto wanaosoma au wasiosoma, wanaweza kusajiliwa pamoja na wazazi au walezi wao kama wategemezi kupitia mpango wa vifurushi vya NHIF vya Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya.

Nitumie fursa hii kuwahamasisha wananchi kuwalipia watoto wao au kujisajili pamoja kama familia ili kupata suluhisho la ugharimiaji matibabu kwa watoto.

Vilevile, Mfuko unatoa huduma kwa makundi mbalimbali ya wananchi katika sekta rasmi na wananchi katika sekta isiyo rasmi ambapo mwananchi anaweza kujisajili kupitia mpango wa vifurushi kwa kutegemea umri wa mchangiaji, idadi ya wanufaika katika familia na mahitaji ya huduma za matibabu.

Pia Mfuko unamwezesha mwananchi kujilipia Kidogo kidogo kupitia mpango wa Dunduliza kupitia benki.

Pambazuko: Uelewa wa Watanzania wengi kuhusu bima ya afya na bima kwa ujumla ni mdogo sana. NHIF ina mpango gani wa kutoa elimu kwa umma ili kukuza uelewa wa sekta hii muhimu?

Isaka: Moja ya jukumu la NHIF ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa wa dhana ya bima ya afya.

Mfuko unatekeleza mkakati wake wa masoko na elimu kwa umma ambapo unatumia njia mbalimbali za kutoa elimu ya bima ya afya kwa umma.

Mfuko umepanga kuendelea kutumia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari, mikutano ya hadhara, mikusanyiko mbalimbali kama kwenye masoko, maonesho, nyumba za ibada na mitandao ya kijamii kuwafikia wananchi popote walipo ili kuielewa dhana ya bima na wajiunge kabla ya kuugua.

Pambazuko: Mabadiliko gani ya sheria au sera yanapaswa kufanyika ili kuleta ufanisi na tija kubwa kwenye sekta ya bima ya afya nchini?

Isaka: Kwanza kabisa NHIF ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria, lakini kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kumesaidia kuja na maboresho makubwa katika eneo hili. Hivyo, sheria hii itakapoanza kutumika, itasaidia kwa kiwango kikubwa.

Pambazuko: Kuna mipango yoyote ya kuanzisha huduma mpya au kuboresha huduma zilizopo?

Isaka: Mfuko umeendelea na uboreshaji wa huduma zake kila inapoonekana inafaa, bila kuathiri uhai na uendelevu wa Mfuko.

Kwa sasa tunafanya maboresho makubwa ya mifumo yetu yatakayowezesha kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanachama na watoa huduma.

Mifumo hiyo ni pamoja na ya utambuzi wa wanachama, usajili, upokeaji na ulipaji wa madai pamoja na upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wanachama na wadau wa Mfuko.

Pambazuko: NHIF imepanga kufanya nini kuhusu kupunguza gharama za bima kwa wanachama, hasa wale wenye kipato cha chini?

Isaka: Mfuko umepanga kuja na vifurushi nafuu

Inaendelea Uk. 22

Ana kwa Ana

Isaka: Sina uvumilivu kwenye rushwa

Inatoka Uk. 21

zaidi ya vilivyopo ili kumpa mwananchi uwezo wa kununua bima.

Aidha, Mfuko utatumia mpango wake wa Dunduliza kumwezesha mwananchi kuchangia bima kidogo kidogo na kuanza kunufaika baada ya kukamilisha lengo.

Pambazuko: Kuna mpango wowote wa kuongeza wigo wa huduma zinazotolewa na NHIF kwa gharama nafuu?

Isaka: Uongezaji wa wigo wa huduma unategemeana na matokea ya tathmini zinazofanyika ambazo ushauri ni maeneo gani yafanyiwe maboresho. Hivyo, suala hili ni endelevu.

Aidha, tathmini mbalimbali zinaendelea kufanywa na

Mfuko na endapo itaonekana kuna haja ya kuongeza huduma yoyote zitaongezwa kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hizo.

Pambazuko: NHIF inafanyaje kazi na vituo vya afya vilivyo vijijini na maeneo yenye huduma duni za afya ili kuhakikisha wanachama wanapata huduma bora?

Isaka: Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kazi kubwa iliyofanya ni pamoja na uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za matibabu.

Hospitali zimejengwa na huduma zimeshushwa mpaka ngazi ya chini kabisa. Mfano mzuri huduma za kitalaam kwa sasa zinapatikana hadi ngazi ya hospitali za wilaya.

Hivyo, kwa wanachama wa NHIF, imekuwa ni habari njema sana kwao kutokana na urahisi wanaoupata katika kuzifikia huduma wanapozihitaji.

Hata hivyo, Mfuko utaendelea kutoa mikopo nafuu kwa vituo vya afya ili viweze kuboresha mazingira ya kutolea huduma na kurahisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.



Pambazuko: Kuna mpango wa kuongeza vituo vinavyotoa huduma za NHIF au kuboresha mkataba na vituo vilivyopo?

Isaka: NHIF husajili vituo kwa ajili ya kuwahudumia wanachama wake. Vituo hivi ni vya serikali, binafsi na madhehebu ya dini.

Zoezi la usajili huwa ni endelevu kutokana na maombi ya wenye vituo au tunapoona mahitaji kwenye eneo husika.

Kwa sasa Mfuko umesajili vituo 9,194 na utaendelea kusajili vituo vya kutolea huduma kulingana na mahitaji.

Pambazuko: NHIF ina mpango gani wa kuboresha mifumo yake ya kidijitali ili kupunguza ucheleweshwaji wa huduma na kurahisisha taratibu za kupata bima?

Isaka: Kama nilivyodokeza hapo awali, moja ya maboresho makubwa yanayoendelea kwa sasa ni eneo la mifumo ambapo usajili wa wanachama utakuwa ni rahisi na kwa njia ya mtandao.

Kwa sasa, Mfuko unaendelea kuboresha mifumo yake ya Tehama ili kuongeza urahisi wa wananchi kuufikia.

Mabadiliko yanayofanyika kwa sasa yanalenga siyo tu

kuhudumia wadau kwa idadi iliyopo sasa, bali kuweza kuhudumia wananchi wote, chini ya utaratibu wa bima ya afya kwa wote.

Miundombinu ya Tehama inafanyiwa maboresho makubwa ili kuleta ufanisi unaotakiwa. Pia, wanachama wanawezeshwa kujihudumia zaidi, kuanzia uandikishaji, ulipaji michango, ufuatiliaji wa huduma wanazopata na kujua vituo vinavyofanya kazi na Mfuko, na huduma zinazotolewa katika vituo hivyo.

Pia, watoa huduma wanawezeshwa kuwasilisha madai kwa njia ya mtandao. Hatua hii imeanza kwa hospitali chache, lakini lengo ni kuondoa kabisa uwasilishaji kwa njia ya fomu za karatasi.

Watoa huduma na waajiri pia wanawezeshwa kuwasilisha taarifa, michango na kufanya usuluhishi kwa njia ya mtandao.

Inaendelea Uk. 23

Isaka: Sina uvumilivu kwenye rushwa

Inatoka Uk. 22

Kadhalika wanapata taarifa mbalimbali zinazowahusu kwa wakati kwa njia hiyohiyo.

Suala la uharaka na usahihi wa kuchakata madai ya watoa huduma limepewa uzito pia, ambapo Mfuko unasimika mifumo ya kusaidia kuchakata madai hayo kwa uharaka na usahihi.

Tunao mpango wa kutumia Artificial Intelligence (AI)- akili mnemba, kwa Kiswahili, ili kuchakata madai na kutambua kwa urahisi viashiria vya udanganyifu.

Kwenye utekelezaji wa haya, tunawahitaji sana watoa huduma washiriki kikamilifu kwa kufanya mabadiliko stahiki kwenye mifumo yao, kwa viwango vilivyowekwa na serikali, ili mifumo yao iweze kusomana na mifumo yetu kwa urahisi.

Kwa hiyo, utaona kuwa, lengo letu kubwa ni kuhakikisha kuwa wadau wetu wanapata huduma pale walipo, kwa kujihudumia wenyewe, na kuhakikisha yale yanayofanyiwa

kazi na Mfuko yanafanyika kwa uharaka na usahihi kupitia mifumo ya Tehama.

Pambazuko: Kuna mipango ya kuanzisha au kuboresha program za simu au tovuti kwa huduma bora zaidi?

Isaka: Mfuko unazo njia mbalimbali za mawasiliano na wadau wake au upatikanaji wa taarifa zake.

Njia hizo ni pamoja na barua pepe, tovuti, kurasa za mitandao ya kijamii, kituo cha huduma kwa wateja ambacho hufanya kazi saa 24.

Mfuko pia unayo Mobile App (kitufe cha simu janja), ambayo wanachama na hata wale wasio wanachama, wanaitumia kupata taarifa mbalimbali na kujipatia huduma zinazotolewa na NHIF bila kuhitaji kufika ofisini.

Njia hizi zote zinaendelea kuboreshwa ili mwanachama au mdau aweze kupata majibu anayohitaji kwa muda mfupi zaidi kulingana na hitaji lake.

Pambazuko: NHIF itachukua hatua gani kuhakikisha uwazi katika michakato yake, hasa katika malipo ya madai ya bima?

Isaka: NHIF inafanya kazi kwa uwazi zaidi na ushirikishwaji wa wadau wake. Malipo ni kati ya mtoa huduma husika na Mfuko ambaye ameingia mkataba wa kuhudumia wanachama wetu.

Inapotokea changamoto yoyote, mtoa huduma

hutaarifiwa na kufanyika mazungumzo kwa lengo la kutatua changamoto iliyojitokeza ikiwemo ya kukatwa kwa madai yasiyo na uhalisia.

Pambazuko: Utapambanaje na tatizo la rushwa ndani ya NHIF?

Isaka: Kwanza kabisa niseme kuwa binafsi sina uvumilivu hata kidogo na yeyote awe mtumishi au mtoa huduma au mwanachama au mwajiri atakayejihusisha na rushwa au udanganyifu.

Kwa watumishi, zipo taratibu za kiutumishi ikiwemo kufukuzwa kazi na taratibu zingine za kinidhamu.

Kwa wanachama na watoa huduma ni pamoja na kufungia usajili wake au kadi ya matibabu na inapobidi kumfikisha katika vyombo vya sheria ili taratibu za mamlaka hizo zichukue mkondo wake.

Katika hili, nitapambana nalo kwa nguvu zote na kwa njia zote ili uhai wa Mfuko uwe endelevu uweze kutoa huduma kwa wananchi kama lilivyo lengo lake.

Aidha, naenda kuimirisha mifumo ya udhibiti iliyopo kwa kuongeza udhibiti kwenye mifumo ya Tehama na kuimarisha Kitengo cha Kupambana na Makosa ya Udanganyifu.

Pambazuko: Je, kuna njia yoyote mpya ya kuhakikisha kuwa wanachama wanaweza kutoa maoni yao kupata mrejesho haraka?

Isaka: Mfuko hupokea mrejesho wa wanachama kupitia njia nilizozitaja hapo za mawasiliano, lakini pia huwa tuna mikutano mbalimbali na wadau wetu na maoni hayo hutumika katika uboreshaji wa huduma zetu.

Mifumo ya Mfuko iliyopo, ambayo nimeitaja, inatoa nafasi kwa wadau kutoa maoni kwa njia ya mtandao, hata kuweza kuona kiwango cha huduma.

Kwa hiyo, wanachama wanaweza kutoa maoni kupitia Mobile App, tovuti, mitandao ya kijamii na mifumo yetu ya kuwahudumia waajiri na watoa huduma za afya.

Inaendelea Uk. 25

Mtoto wa Mvuvi



Na Maregesi PAUL

Poleni sana familia ya Mzee Kibao



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni (kulia), akimsikiliza Mariam Kibao ambaye ni mtoto wa marehemu Mohammed Ali Kibao, alipotembelea nyumba kwao jijini Tanga hivi karibuni. (Picha na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi)

HEBU fikiria kuwa Mohammed Ali Kibao ni baba yako mzazi.

Asubuhi kulipokucha, akakupigia simu kukusalimia, kisha mkaongea mambo mengi yanayohusu familia zenu.

Kisha akakuambia kwamba siku hiyo jioni atasafiri kwa basi kwenda Tanga ili akakamilishe baadhi ya mambo yake huko, kisha arudi tena Dar es Salaam kwa ajili ya kuendelea na shughuri zake za kichama pamoja na mambo mengine yanayomfanya aendelee kuwapo jijini.

Kwa kuwa ni baba yako mzazi na huyo ndiye 'jembe' lako, kama watoto wa mjini wanavyopenda kusema, unamtakia safari njema na kumkaribisha nyumbani kwako pindi atakapokuwa amerudi Dar es Salaam akitokea Tanga.

Unaagana na baba yako, unamkumbusha jinsi wajukuu zake ambao ni watoto wako wanavyomkumbuka, kisha unakata simu na kuendelea na shughuli zako za kila siku.

Kabla jua halijazama, unachukua simu janja yako, unaangalia makundi sogozi uliyomo, unakutana na habari kwamba, baba yako huyo ameshushwa kwenye gari alilokuwa amepanda, akafungwa pingu na kuchukuliwa na "watu wasiojulikana" waliokuwa na bunduki.

Unaanza kulia kwa uchungu kimya-kimya, unashika Biblia yako au Quran, kisha unaanza kusali kumuombea baba yako ili Mungu aingilie kati na hatimaye 'jembe lako' apatikane akiwa mzima wa afya.

Kisha, saa chache baadaye, wakati ukiendelea na maombi kwa uchungu na maumivu yaliyopitiliza, unapata taarifa kwamba, mwili wa baba yako umeokotwa vichakani ukiwa ameumizwa vibaya baada ya kuuawa na watu hao wasiojulikana.

Naamini hiyo itakuwa ni moja ya habari mbaya ulizowahi kuzisikia katika maisha yako kwa sababu hakuna anayetamani kusikia mzazi wake au mtu yeyote wa karibu naye, anapata matatizo ya aina hiyo kama yaliyoipata familia ya Mzee Kibao.

Familia ya Mzee Kibao inapitia katika kipindi kigumu, watoto wake wanalia kwa uchungu usiokuwa na mfano, mkewe anaugulia maumivu yasiyokuwa na kipimo na hali kadhalika, ukoo wa marehemu, ndugu jamaa na marafiki, wanasikitika na kuumizwa sana baada ndugu na rafiki yao kuuawa kikatili.

Kutokana na hilo, nawapa pole familia ya Mzee Kibao, nawapa pole wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambako marehemu alikuwa akihudumu kabla ya kifo chake na pia nawapa pole Watanzania wote walioumizwa na tukio hilo.

Kilichobaki sasa, ni sisi tuliobaki hai tuendelee kukemea mauaji ya aina hiyo na mengine yasitokee tena kwa sababu yanachafua sura ya nchi yetu katika ramani ya dunia.

Wenye uwezo wa kusali kwa namna yoyote wanayojua wafanye hivyo, wenye uwezo wa kuswali wasichoke kufanya hivyo na hata wenye mamlaka ya kuchunguza chanzo cha tukio hilo na mengine ya aina hiyo, wasiogope kutimiza wajibu wao ili wahusika watakapopatikana, wachukuliwe hatua wanazostahili kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

Isaka: Sina uvumilivu...

Inatoka Uk. 23

Pambazuko: NHIF inashirikianaje na serikali katika kuhakikisha kuwa sheria mpya ya bima ya afya kwa wote inafanya kazi kwa ufanisi?

Isaka: Sheria iliyoanzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ikisomwa pamoja na Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inatambua taasisi mbalimbali za serikali kuwezesha Mfuko kufanya kazi kwa ufanisi.

Katika kuhakikisha sheria mpya ya Bima ya Afya kwa Wote inafanya kazi kwa ufanisi, NHIF inafanya mambo kadhaa ikiwamo kuzingatia miongozo na Sera za Afya zinazotolewa na na Wizara ya Afya ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kwa utaratibu wa bima.

Pia kuimarisha uhusinano na mawasiliano ya karibu na Wizara ya Fedha inayokusanya michango ya asilimia tatu kwa wafanya kazi, asilimia tatu kwa waajiri na kuwasilisha kwa Mfuko kuwezesha malipo kwa watoa huduma, uwekezaji na uendeshaji bora wa Mfuko.

Tumejikita pia kutekeleza miongozo inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Bima nchini, iliyoko chini ya Wizara ya Fedha, kuhakikisha wanachama wanapata huduma bora na kunakuwa na uhimilivu na uendelevu wa Mfuko.

Kwa upande mwingine, tunaendelea kusajili wanachama kutoka sekta binafsi ili kuunga juhudi za Wizara ya Viwanda na Biashara inayoweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, ambapo sekta binafsi inashamiri na kuwawezesha wananchi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kufanya biashara na kujiunga na Bima ya Afya.

Tuna kazi pia ya kuimarisha matumizi ya Tehama kwa kuzingatia miongozo ya Wizara ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inayowezesha kutengeneza mifumo ya Tehama kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Mfuko.

Tuna jukumu pia la kuzingatia miongozo ya uwekezaji inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania katika kuwekeza fedha za ziada za Mfuko ili kuhakikisha Mfuko unapata faida na kuendelea kuhudumia waanachama kwa ufanisi.

Aidha, Mfuko unaendelea kutumia vizuri uwekezaji wa Serikali za Mitaa kupitia uwepo wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambazo zinamiliki hospitali na vituo vya kutolea huduma na kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wanachama wa Mfuko.

Pambazuko: Kuna mipango yoyote ya kuongeza ushirikiano na sekta binafsi ili kuboresha huduma?

Isaka: Mfuko unakiri kuwa sekta binafsi ni mdau muhimu katika kufanikisha azma ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambapo sekta hii imeajiri wafanyakazi ambao watakuwa na bima ya afya na pia inamiliki vituo ambavyo vinatoa huduma kwa wanachama wote wa Mfuko.

Hivyo, Mfuko umepanga kuimarisha uhusiano na sekta binafsi na kuhakikisha kuendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa maslahi ya pande zote.

Pambazuko: Ni changamoto gani kubwa unazoziona katika sekta ya afya Tanzania kwa ujumla na kwenye eneo la bima ya afya, na NHIF inachukua hatua gani kukabiliana nazo?

Isaka: Changamoto kubwa ni uhiari wa wananchi kujiunga na kutoielewa dhana ya bima ya afya.

Aidha, kukithiri kwa vitendo vya udanganyifu kwa wadau, ikiwemo baadhi ya wanachama, waajiri na watoa huduma na gharama zinazotokana na magonjwa sugu yasiyoambukizwa.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Mfuko unaendelea kutoa elimu kwa wananchi kujiunga kwa wingi na huduma za bima ya afya kabla ya kuugua, kujiepusha na vitendo

vya udanganyifu na kuweka mifumo ya kukabiliana na vitendo hivyo ili Mfuko uendelee kuwa hai na endelevu.

Pambazuko: NHIF imepanga vipi kushughulikia suala la upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba kwa wanachama wake?

Isaka: NHIF inafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na wadau wake, ikiwamo Bohari ya Dawa (MSD) na watoa huduma wengine.

Tunapoingia mkataba na mtoa huduma, anatakiwa kuhakikisha huduma zote zilizopo kwenye mkataba anazo na anawapa wanachama wetu. MSD ndio mwenye dhamana hasa ya eneo hili.

Mfuko utaendelea kutenga fedha za mikopo kwa watoa huduma ili waweze kuchukua mikopo hii na kuboresha majengo, upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na kuhimarisha mifumo ya Tehama.

Habari

Sifa za anayefaa kuongoza Tanzania

Inatoka Uk. 4

Ilani hiyo inaainisha sifa nyingine kuwa ni lazima awe na utashi na busara za kiuongozi na asiyekubali kupitisha na kusimamia sheria mbovu zenye kukandamiza utawala bora, demokrasia na haki za binadamu.

"Kiongozi wa Tanzania tuitakayo lazima awe ni muwazi katika utendaji kazi wa serikali na anayethamini ushirikishwaji wa wananchi katika mipango ya umma kwa maendeleo ya Taifa..."

"Pia anapaswa kuwa muumini wa maendeleo shirikishi yatakayoweza kuinua uchumi na kutengeneza mazingira rafiki ya ajira kwa maendeleo endelevu..."

"Lazima awe muwajibikaji na aliye tayari kufanya uamuzi wenye tija kwa taifa pamoja na kuwawajibisha viongozi wengine wa umma wanaposhindwa kutekeleza majukumu yao bila kuvunja sheria za nchi," inasomeka sehemu ya Ilani hiyo.

Vilevile ilani inataja vipaumbele vikuu vya asasi hizo kuwa ni katiba mpya, kuundwa kwa sera ya uchumi jumuishi na maendeleo endelevu, usimamizi wa rasilimali za umma na kutokomeza rushwa.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, Lema alizipongeza asasi hizo kwa kuandaa mapendekezo ya ilani hiyo, akisema wamefanya kazi kubwa.

"Kwa niaba ya chama changu natoa pongezi kwa kusanyiko lililokutana kuandaa hizi nyaraka kwa kweli zimefanya kazi ya maana sana..." "Hatari kubwa sana inayoikabili ulimwengu ni kukosekana kwa nia njema, kwa hiyo mapendekezo kama haya yanaweza kukosa nafasi," alisema Lema.

Kwa upande wake, Katibu wa Idara ya Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa wa CCM, Rabia Abdallah, alizipongeza asasi hizo na kusema kuwa chama chake kimeyapokea mapendekezo hayo ya ilani kwa uzito mkubwa..."

"Mmeonyesha ni kwa kiasi gani serikali iongoze na iwasikilize. Sisi tunakwenda kuyaheshimu maoni haya na CCM kimejiandaa



Onesmo Olengurumwa

kupita kwenye makundi ya kijamii kuchukua maoni nini wanataka kuona serikali inafanya, sasa hili andiko limetupa kwa mwongozo," alisema Rabia.

Kuhusu ujenzi wa amani nchini, Ilani hiyo inasema kuwa ingawa amani imekuwepo kwa miaka mingi, bado

imeendelea kugubikwa na vitendo vinavyoathiri haki za kiraia na kisiasa kama vile mauaji, uminywaji wa uhuru wa vyombo vya habari, vurugu, vikwazo vya upatikanaji wa haki, na changamoto za mfumo wa haki jinai.

Ilani inaanisha kuwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana, lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanya, kwani katika kipindi cha miaka mitano tangu kutolewa kwa ilani ya Azaki ya uchaguzi ambayo iliweka matamko mahususi ya uimarishwaji wa haki za kiraia na kisiasa, Tanzania imepita katika vipindi mbalimbali ya kupanda na kushuka

katika viwango vya kimataifa pamoja ulinzi wa haki za binadamu.Mathalan, ilani inaeleza kuwa kati ya mwaka 2021 na 2022 Tanzania ilipanda kwa nafasi moja katika viwango vya kielelezo cha uhuru wa vyombo vya habari duniani

kwa mujibu wa Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka (RSF), hata hivyo, mwaka 2023 Tanzania ilishuka kwa kiasi kikubwa kwa nafasi 20 hadi nafasi ya 143.

Mapya, magumu mauaji ya Kibao

Inatoka Uk. 8

Kamanda Polisi Jamii

Mkazi wa Ununio, Goma Waziri, ambaye pia ni Kamanda Mkuu Polisi Jamii Kata ya Mbweni, ameliambia Pambazuko kuwa yeye alikuwa anapita eneo hilo majira ya saa moja kasoro asubuhi kwa pikipiki siku hiyo ya Jumamosi, Septemba 7, akaona watu wamekusanyika wakiwemo bodaboda, hali iliyomsukuma kujua kulikoni mkusanyiko huo?

"Nilisogea na kukuta watu wakishangaa mwili wa mtu mwenye asili ya Kiarabu ukiwa umelala kifudifudi kando ya barabara ukiwa umefunikiwa kwa kipande cha zulia la plastiki kuanzia kichwani hadi mgongoni.

"Nilipouangalia, ulionekana ni mwili wa mtu aliyeshambuliwa na kuteswa mahala fulani kisha kuja kutupwa hapa..."

"Alikuwa amevaa suruali ya rangi ya khaki, ambayo hata hivyo ilikuwa chini ya kiuno, viatu vyeusi vilivuliwa na kuwekwa kando na shati la miraba myeusi na myeupe lilikuwa limevuliwa likabaki kwenye mkono mmoja..."

"Nilichukua hatua ya kupigia Mkuu wa Upelelezi wa Polisi Mbweni (OC-CID) ambaye hakukawia, alifika mara moja akiwa na timu yake," alisema.

Alisema baada ya polisi kufika waliliziba eneo hilo kwa utepe na kuanza kazi yao, ambapo waliufunua mwili wenyewe, kisha waligeuza. Sura ilikuwa imeharibiwa vibaya na alishuhudia, macho yalikuwa yametobolewa, muathiriwa alikuwa "hatazamiki mara mbili usoni."

Goma alisema baada ya polisi kumaliza kazi yao, waliwaita wananchi waliokuwa eneo hilo na kuwauliza kama kuna mtu anayeweza kumtambua, walisimamisha hadi baadhi ya magari ya watu wenye asili ya Kiarabu kuwaonyesha kama wanaweza kumtambua, lakini hakuna aliyeweza kumtambua.

"Baada ya hapo waliupakia mwili kwenye gari ya polisi na wakaupeleka Hospitali ya Mwananyamala ambapo ulikwenda kuhifadhiwa. Siku ya pili ndiyo tukasikia kuwa kumbe ule ulikuwa ni mwili wa kada wa Chadema aliyetajwa kwa jina la Kibao," alisema.

Alieleza kuwa eneo hilo limekuwa na matukio mabaya, ikifika usiku kuanzia saa moja watu wanaogopa kupita hapo kwa sababu upende mmoja una vichaka na misitu ya mikoko na upande mwingine una viwanja vya watu ambavyo havijaendelezwa, kunakuwa na kiza totoro..."

"Hata madereva wa bodaboda wanaliogopa, wanapita kwa tahadhari sana, bahati mbaya hata sisi watu wa ulinzi shirikishi na polisi jamii huwa siyo rahisi kufika huku nyakati za usiku kwa sababu ya namna eneo lilivyo, ni parefu sana, labda hadi tusikie kuna tukio,"aliongeza.

Alisema wanaomba, ili kuimarisha usalama eneo hilo, angalau lingewekwa taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua (sola) zingesaidia, maana ikifika usiku angalau lingekuwa na mwanga.

Pia alisema wanaomba wapatiwe vitendea kazi ili viwasaidie kuimarisha ulinzi shirikishi, wakazi wa eneo hilo wanaweza kuwasaidia hata pikipiki mbili kupitia Serikali ya Mtaa ambayo itawezesha uimarishaji wa ulinzi kwa sababu eneo hilo baadhi ya wenye maeneo yao wana walinzi, lakini hawasaidii sana katika kudhibiti matukio ya uhalifu.



Mmoja wa akinamama wauza chenji, akisubiri wateja ambao ni makondakta wa daladala kwa ajili ya kuwauzia, ambapo chenji ya sh. 1000 huuzwa kati ya sh. 150 hadi 200 kama alivyokutwa katika kituo daladala Mbezi, Jijini Dar es Saalam mwishoni mwa wiki. (Picha na Fidelis Felix)

Riwaya

Viaticum-6

Sakramenti ya Mwisho



Hatimaye Eddy amefika Mwanza na kuanza misele yake ya kuelekea kanisani, huku kichwa bado kimejaa mawazo, ni nini hasa kitatokea huko? Endelea kusoma riwaya hii "tamu..."

Na Godwin Chilewa, Houston, MAREKANI

BAADA ya kuoga akatoa nguo alizoziandaa kwa ajili ya siku hiyo; suti nyeusi, shati jeupe, tai nyekundu na viatu vya ngozi nyeusi. Alichagua nguo hizi makusudi kumuonesha mtu aliyemualika jinsi alivyoithamini siku hii.

Kwa Wakatoliki, rangi nyeusi huwakilisha msiba au maombolezo. Rangi nyekundu huwakilisha damu ya watakatifu iliyomwagika katika kumtangaza Kristo, na rangi nyeupe ni ishara ya utakatifu wanaopokea waaminio kwa neema na msamaha wa dhambi katika Kristo Yesu.

Alipomaliza kuvaa, akajipulizia marashi, akaweka vitu sawa, akafunga sanduku na kulirudisha kabatini. Ndipo akatoka chumbani na kufunga mlango.

Mapokezi alimkuta muhudumu aliyempokea na kumuonesha chumba alicholala. Alikuwa msichana mrembo mwenye umri usiozidi miaka ishirini na tano.

"Ng'wangaluka sanchi? Eddy alimsalimu kwa lugha ya Kisukuma huku akitabasamu.

Binti wa watu akaangua kicheko cha furaha. Hakutegemea kama mgeni wake angemsalimu kwa lugha ya kwao.

Uzoefu alioupata akiwa kazini ulimuwezesha kuwatambua wateja wenyeji, na wale wanaotoka nje ya Kanda ya Ziwa kwa lafudhi zao tu. Ingawa Eddy alichagua maneno sahihi, sauti na rafidhi yake vilimsaliti.

"Nilipokuona tu nilijua wewe siyo mwenyeji wa Mwanza," mhudumu huyo alisema huku akiendelea kucheka.

"Ni kweli mimi si mwenyeji wa hapa, lakini nimeazimia kuoa Msukuma, kwa hiyo lazima nijifunze lugha ya wakwe," Eddy alijibu huku akicheka.

Basi, wakatupiana maneno mawili matatu ya utani kisha Eddy akamuaga na kuondoka.

Alipotoka nje akaiona gari aina ya Nissan Altima, nyeupe imeegeshwa umbali wa mita ishirini hivi kutoka lango la mbele.

Frank alikuwa amesimama pembeni yake akiisafisha vioo kwa kitambaa.

"Habari za asubuhi Frank?"

"Njema sana bosi wangu, pole kwa uchovu wa safari."

"Ahsante sana, najisikia vyema."

"Ulipata mwenyeji? Frank aliuliza huku akitabasamu.

"Bado sijapata, mimi ni mtu wa subira sana!" Eddy alijibu akitabasamu.

"Ni kweli nyie wakubwa huwa hamna haraka ya maisha, mambo yanawanyookea bila kukunja ngumi," Frank alijibu huku naye akicheka.

Eddy hakuongeza neno lolote. Ubongo wake ulishaanza kufungua mafaili ya kumbukumbu za shida, vurugu na vitisho anavyopambana navyo mara kwa mara bila wengine kujua yanayomsibu.

Akaingia kwenye gari na kufunga mkanda. Frank naye akaingia na kuwasha gari, wakaondoka kuelekea Bugando.

Muda huu msongamano wa magari ulikuwa bado haujaanza. Frank akaendesha kwa kasi katika Barabara ya Kapripointi inayopita mbele ya jengo la chuo cha benki.

Inaendelea Uk. 29

Riwaya

Viaticum-6

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

Mbele kidogo akakata kona kushoto kufuata Barabara ya Stesheni, akaendesha moja kwa moja mpaka kwenye makutano ya Barabara ya Mkuyuni.

Hapo akanyoosha mpaka walipokutana na Barabara ya Nyerere. Akapunguza mwendo, akakata kulia kufuata barabara hiyo.

Barabara ya Nyerere huwa na msongamano wa magari muda wote, kwani ndiyo inayotumika kwenda Nairobi, Kenya, kupitia Magu, Bunda, Tarime hadi Sirari.

Kwa hiyo Frank akalazimika kupunguza mwendo. Walipofika njia panda akaingia Barabara ya Pamba, halafu mbele kidogo akakata tena kushoto kufuata barabara inayokwenda kanisa kuu la Epifania Bugando.

Wakati akiegesha gari kwenye maegesho ya kanis, mishale ya saa iliyo kwenye dashibodi ya gari ilionesha imeshatimia saa moja kasoro dakika ishirini na nne asubuhi. Eddy akampa ujira wake, wakaagana.

Kanisa Kuu la Epifania limejengwa karibu na Hospitali Kuu ya Rufaa Bugando ambayo pia ni ya Kanisa Katoliki. Kanisa hili ndilo lililokuwa makao makuu ya Jimbo Kuu la Mwanza kwa miaka mingi kabla ya kuhamishiwa Kawekamo.

Waliolijenga waliamua kulipa jina la Epifania kwa heshima ya kumbukumbu ya Epifania ya Bwana, nyota iliyowaongoza wataalam wa nyota (Mamajusi) kutoka mashariki, kwenda kumtembelea Mtoto Yesu (Mathayo 2:2).

Wanatheolojia hufafanua kwa kusema nyota hiyo ilikuwa ni ishara ya kipekee kwamba Mungu huwaelekeza kwenye wokovu watu wa nyakati zote, wakati wote na mahali pote.

Katika Kanda ya Ziwa Victoria, dini ya Kikristo hususan Ukatoliki uliletwa na kikundi cha wazungu (White Fathers) zaidi ya miaka mia moja iliyopita.

Jitihada kubwa walizozifanya ndizo zilizochangia kuenea kwa Ukatoliki kwa kasi katika kanda hiyo. Leo hii Ukatoliki umeota mizizi kila mahali kiasi cha kuzaliwa majimbo mengi, yenye nguvu kubwa kiimani, kiuchumi na kisiasa chini ya maaskofu wake.

Majimbo hayo ni pamoja na Bukoba, Geita, Musoma, Rulenge na Shinyanga; haya yote yakiwa chini ya Jimbo Kuu la Mwanza ambalo makao makuu yake yalikuwa Bugando, kabla ya kuhamishiwa Kawekamo.

Wakati Eddy akiingia ndani kanisa, tayari lilikuwa limeshaanza kujaa. Hiyo ilimpa dalili kwamba watu wa Mwanza ni wacha Mungu, wanaojali ibada.

Baada ya kuangalia huku na kule akaona nafasi wazi kwenye benchi la pili kutoka nyuma, karibu kabisa na mahali wanapopita mapadre kutoka altareni.

Akaiendea nafasi hiyo, akapiga magoti mbele ya benchi, akasali sara fupi, kisha akainuka, akakaa kwenye benchi kusubiri.

Kanisa lilikuwa limepambwa vizuri maalum kwa siku ya watakatifu. Sehemu yote ya mbele pamoja na altare ilipambwa kwa vitambaa vya rangi nyeupe vilivyotalizwa kwa nyuzi za rangi ya dhahabu.

Pembeni, upande wa pili wa kanisa walikeeti watawa wa kike (masista) wapatao ishirini na nne waliovaaa mavazi meupe yaliyowafanya waonekane kama malaika.

Mpaka wakati huo, kwaya ilikuwa bado haijaanza kuimba. Mpiga kinanda ndiye aliyekuwa akitoa burudani kwa kupiga kwa ufundi nyimbo nzuri za kumsifu Mungu.

Mbele madhabahuni alikuwepo shemasi mmoja, na wahudumu wengine wawili wakikamilisha maandalizi ya misa kwa kuwasha mishumaa na kupanga vyombo vya sakramenti mezani.

Itaendelea wiki ijayo...Usikose



Habari

Wanasubiri nini kujiuzulu?

Inatoka Uk. 19

Kiongozi huyo wa kiroho amesema matendo haya yanapoongezeka na wanaolengwa zaidi wakiwa ni wale wenye mitazamo tofauti na serikali, au chama tawala, basi kuuawa kunatia shaka kama kweli wenye dhamana ya kulinda uhai wa binadamu wanafanya kazi wanazowapaswa kufanya kwa weledi na haki.

Amesema wakati umefika sasa kwa viongozi wenye dhamana ya kulinda uhai wa Watanzania, lakini huku wananchi wanaendelea kuteswa na kufa, sasa wajitathmini na ikiwezekana waonyeshe kuwajibika kwa kuachia ngazi.

Joseph Butiku akemea

Jumanne Septemba 10, 2024, Joseph Butiku, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Mwalimu Nyerere, alisema Masauni na Wambura wanapaswa kuondoka madarakani kwa kulinda heshima zao, lakini pia kwa kuonekana kuwa wanawajibika.

Alisema tatizo la mauaji, kuteka watu, kunyanyasa watu halikuanza leo, wala halikuanza na huyu (Kibao) bali lilianza wakati wa Rais John Magufuli, na huko nyuma kabla hata wakati wa Serikali ya Awamu ya Kwaza chini ya Mwalimu Julius Nyerere.

Amesema, lakini wakati wa Mwalimu aliwaadhibu, ambapo hata aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Ali Hassan Mwinyi alijiuluzu kwa sababu watu wa usalama walifanya mambo yasiyostahili.

"Mnakumbuka Mwalimu alisafisha Jeshi la Polisi mara moja; akaliengua lote akajenga linguine. Mnakumbuka Idara ya Usalama ilishawahi kutenguliwa yote viongozi wao wote wakaondolewa wakawekwa wengine.

"Mnakumbuka Mzee Natepe (Abdallah) alikuwa waziri, na wakati wake, kuna watu walitoroka magerezani; hakuwatorosha yeye, lakini alilazimika kuwajibika. Kwahiyo, jambo la kuwajibika naona kama linafifia.

"Huwezi kuwa na watu wanakufa, wanaelea kila mahali kwenye maji – kwenye Bahari na nini, halafu wewe ni waziri upo tu unasema rais ameagiza, unangoja akuagize? Tayari amekupa kazi. Wajibika. Usingoje kusema tu Rais, Rais ameagiza.

"Kazi ya Rais ni kuambiwa ili aagize, lakini kabla ya kuagiza yeye atakuwa amepata taarifa kutoka kwako. Kwa hiyo wajibu wa kwanza ni wa kwako," alisema Butiku.

Msaidizi huyo wa Mwalimu Nyerere alisema haiwezekani matukio makubwa na yenye kuogopesha yanatokea kila mara na mengine yakifanyika chini ya mitutu ya bunduki za kivita, yakatokea bila viongozi wakuu wa vyombo vya usalama kuwa na habari. Hivyo, ni muhimu wapumzike.

Alisema haiwezekani viongozi hao wasiwajue hao walioingia kwenye basi na kumchukua Kibao ni akina nani? Ni wanaume wa nani? Wanawajua. Wanajulikana na kwamba, ushauri wake anaoutoa "kwa unyenyekevu" - akiwa mzee, ni kutaka wanaohusika wawajibike.

Mabalozi EU wanena


Jumanne Septemba 10, siku moja baada ya Kibao kuzikwa, mabalozi wa nchi za Umoja wa Ulaya, pamoja na mabalozi wa nchi za Canada, Norway, Uswisi na Uingereza, walitoa tamko la kuonesha kusikitishwa na matukio ya ukatili, kupotea kwa watu na vifo vya wanaharakati wa kisiasa na haki za kibinadamu nchini Tanzania.

"Tunatoa mwito wa kufanyika kwa uchunguzi wa kina kuhusu matukio haya. Tunatoa pole kwa familia zote zilizoathiriwa. Tunahimiza serikali ya Tanzania kuhakikisha ulinzi wa upinzani, kama alivyoahidi Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia mpango wake wa '4R', na kwa mamlaka kuchukua jukumu la kulinda haki za msingi za wananchi, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kujielekeza," imeeleza zaidi taarifa hiyo.

Mabalozi hao walieleza kuwa wanakaribisha wito wa Rais wa kufanya uchunguzi wa haraka ili kubaini wahalifu waliohusika; na kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji.

Inaendelea Uk. 32

Kenya kugeuka taifa la migomo



Rais wa Kenya, William Ruto

Na Julius MKAMBI, Nairobi

SIYO madaktari, wala waalimu wa sekondari, na siyo wakufunzi wa vyuo vikuu, wala wanafunzi wa vyuoni, na hata wahudumu wa viwanja vya ndege, swali la kujiuliza ni je, Kenya sasa inaanza kugeuka kuwa taifa la migomo?

Migomo kwenye sekta mbalimbali, tena za umma zinakuja katika kipindi ambacho Kenya imeshuhudia maandamano yaliyoitikisa Serikali ya Rais William Ruto kiasi cha kulazimika kuvunja baraza lake la mawaziri.

Japo Rais Ruto aliteua baraza jipya akijumuisha baadhi ya viongozi waandamizi kutoka chama cha upinzani kinachoongozwa na Raila Odinga, bado lipo kundi la Wakenya ambalo halijaridhishwa.

Kundi hili linajumuisha vijana wa Gen Z ambao kwa kiasi kikubwa walihamasishana kupitia mitandao ya kijamii, kufanya maandamano ya kupinga Muswada wa Fedha 2024 na pia kutaka Rais Ruto kuwajibika kwa kutekeleza ahadi zilizotolewa wakati wa kampeni.

Maandamano ya Gen Z yalifuatiwa na yale ya waansishi wa habari wakilalamikia Jeshi la Polisi kuwanyanyasa na kuwashambulia wakati wakitekeleza majukumu yao kuhabarisha yanayojiri kwenye maandamano ya Gen Z.

Awali taifa lilishuhudia maandamano ya madaktari wakishinikiza serikali kutekeleza makubaliano waliyotia saini mwaka 2017 kuhusu nyongeza ya mishahara na fedha kupewa kwa wanafunzi ambao wapo kwenye mafunzo ya vitendo.

Wakati haya yote bado hayajapoa, wafanyakazi wa serikali za kaunti - Septemba 3 mwaka huu, walitoa notisi ya siku 21 kufanya mgomo kulalamikia mishahara yao kutofanyiwa mapitio, kwa lengo la kuongezwa.

Serikali za kaunti ambazo hazina tofauti na majimbo, zilibuniwa kufuatia kupitishwa kwa Katiba mpya mwaka 2010 na utekelezaji wake ulianza rasmi baada ya uchaguzi mkuu mwaka 2013.

Lengo la kuanzisha serikali za kaunti ilikuwa ni kusongesha huduma karibu na wananchi japo kumekuwa na ripoti nyingi kuhusu ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha za umma, huku magavana wakinyooshewa kidole kuishi maisha ya anasa.

Katibu Mkuu wa Muungano wa Wafanyakazi wa Serikali za Kaunti Kenya, Roba Duba, alitaja ukosefu wa mapitio ya mishahara tangu 2012 kuwa sababu kuu ya kuitisha mgomo huo.

Hali hii inaelezwa kutishia na kuhatarisha utulivu wa nchi wakati taifa limetoka tu kupata ahueni kutokana na kuepusha migomo iliyoitishwa na madaktari na walimu.

Tume ya Mishahara na Marupurupu (SRC) iliongeza zuio la nyongeza ya mishahara kwa maofisa wote wa umma na kufifisha matumaini ya maelfu ya wafanyikazi wa serikali wanaotaka kuboreshwa kwa mishahara.

Kulingana na SRC, hatua ya kusitisha ukaguzi wa mishahara ilitokana na matatizo ya kifedha yanayokabili Hazina kwa kuzingatia kuongezeka kwa majukumu ya ulipaji wa deni na kukosa ukusanyaji wa mapato.

Habari



Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Michael Battle

Wanasubiri nini kujiuzulu?

Inatoka Uk. 30

Ubalozi wa Marekani walonga

Taarifa ya mabalozi hao ilikuja siku moja tangu Ubalozi wa Marekani kutoa tamko lake Septemba 9,2024, tamko lililoambatana na salamu za rambirambi kufuatia mauaji ya kiongozi wa Chadema, Kibao.

"Marekani inaungana na wale wanaotoa wito wa uchunguzi huru, wa wazi na wa haraka kuhusu utekaji unaoendelea na mauaji ya Ali Mohamed Kibao," ilieleza sehemu ya tamko hilo.

"Marekani ilieleza kuwa mauaji na kupotea kwa watu, pamoja na kukamatwa, kupigwa, na vitendo vingine vya kuwaengua raia katika uchaguzi vilivyotokea mwezi uliopita, havipaswi kuwa na nafasi katika demokrasia. Vitendo hivi vya kikatili vinadhoofisha haki zinazohakikishwa na Katiba ya Tanzania.

"Tunatoa rambirambi zetu za dhati kwa familia ya Bwana Kibao na kwa taifa kwa kupoteza maisha yake na uongozi wake wa kiraia."

Wanasheria TLS wakasirishwa

Tamko la TLS lililotolewa Septemba 10, 2024 kupitia kwa rais wao, Boniface Mwabukusi, lilieleza kusikitishwa na hivyo kulaani kitendo cha utekaji na kuuawa kikatili kwa Mohammed Kibao, likivikumbusha vyombo vya dola juu ya majukumu yake ya kikatiba na kisheria ya kulinda watu na mali zao.

Tamko lilieleza kuwa kumekuwa na ongezeko la watu kutekwa na baadaye kupatikana wameuawa; kitu ambacho ni kinyume cha Katiba na ni kinyume cha mikataba ya kimataifa, likiwamo Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu.

TLS ilitoa mwito kwa Rais Samia kuunda tume huru itakayochunguza matukio ya kupotea, kutekwa na kuuawa kwa wananchi ili kupata ufumbuzi wa kudumu; na kurejesha imani ya wananchi juu ya uhuru wao na haki za msingi za Kikatiba ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi ambayo sasa iko shakani.

Pia Mwabukusi iliwataka Masauni, Wambura, na Mkuu wa Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Awadh Haji, kuwajibika kwa kujiuzulu.

TLS imeeleza kuwa imeona sheria zilizopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zinatoa mianya kwa vikundi, taasisi au watu fulani kufanya kazi zao bila kuzingatia misingi ya haki nchini.

Kwa msingi huo, TLS imeeleza kuwa inapitia sheria hizo, na itazifikisha mahakamani kuzipinga kwa msingi wa sheria na Katiba; na kwamba inavitaka vyombo vyote vya dola kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi.

LHRC yakemea

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kilitoa tamko, siku moja baada ya kutekwa na kuuawa kwa Kibao kikitaka kufanyika uchunguzi wa kina kubaini wahusika wa mauaji.

Pamoja hilo, kituo hicho kiliwataka wasimamizi wa vyombo vya dola, akiwamo Masauni, kujiuzulu.

Kiliisihi serikali kufanya uchunguzi wa kina na haraka, kubaini wahusika na kuwachukulia hatua; uchunguzi huo uwe wa wazi na mamlaka husika zielekeze juhudi kwenye kudhibiti matukio ya namna hiyo ili kupunguza taharuki kwa jamii.

"Jeshi la Polisi lidhibiti mianya ya uhalifu ndani ya vyombo vya dola; lihakikishe watu wasiokuwa na dhamana hawapati nafasi ya ku-

Inaendelea Uk. 33

Wanasubiri nini kujiuzulu?

Inatoka Uk. 32

jipenyeza na kutenda uhalifu wakijifanya sehemu ya vyombo vya ulinzi," kituo kilieleza katika taarifa yake kwa umma.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyosainiwa na Mkurugenzi Mtendaji wake, Anna Henga, LHRC imetoa rai kwa Rais Samia Suluhu Hassan kutoa tamko la kukemea matukio hayo ya utekaji na mauaji yanayoendelea nchini.

ACT-Wazalendo

Chama cha ACT-Wazalendo nacho, kililaani tukio hilo, kikisema linaongeza hofu juu ya usalama na amani nchini.

"Tunajiuliza, hivi ni nani anayeweza kufanya matukio haya siku zote hizo bila kukamatwa? Je, vyombo vyetu vinazidiwa uwezo na watekaji? Majibu ya wananchi ni kudai kuwa vyombo vyetu ndivyo vinahusika. Sasa tunajiuliza, utekaji huu unafanyika kwa masilahi ya nani? Na kwa lengo lipi?" imehoji ACT.

Zitto Kabwe, Kiongozi (mstaafu) wa ACT-Wazalendo, kupitia ukurasa wake wa X (zamani Twitter) amelaani tukio hilo na kumtaka Rais Samia kuchukua hatua ikiwemo kuunda tume ya kijaji ili kuchunguza tukio hilo la Kibao na matukio mengine ya watu wanaopotea au kutekwa.

CCM yatia neno

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimezungumzia matukio ya kutekwa, kuteswa na hata kuuawa kwa baadhi ya Watanzania na kutamka kuwa, wote wanaohusika wasakwe na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Dkt. Emmanuel Nchimbi amesema kuwa chama chake hakipendezwi na matukio ya kutekwa na kuuawa kwa Watanzania na kwamba wanaoendesha na kutekeleza matukio hayo wanachafua taswira ya chama hicho tawala.

Rostam Aziz

Jumatatu Septemba 9, 2024 siku ambayo Kibao alizikwa, Mfanyabiashara maarufu na kada wa CCM, Rostam Azizi, aliungana na Watanzania wengine kulaani vikali mauaji ya Kibao, akielezea masikitiko yake makubwa kufuatia tukio hilo la kikatili, akisema ni hatua ya taifa kurudi nyuma.

"Nchi yetu imejengwa kwenye misingi ya utu, uhuru na haki. Matukio ya kikatili kama haya hayapaswi kupewa nafasi katika jamii yetu," alisema Rostam katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Rostam, ambaye amewahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi nchini, ametoa mwito kwa Watanzania wote kushikamana na kuhakikisha kuwa taifa linaendelea kusimamia misingi ya haki na usawa kwa kila mtu.

"Tusiruhusu kurudi nyuma kwenye giza la ukosefu wa utu na thamani ya maisha ya binadamu," aliongeza.

Wageuka bubu

Hadi gazeti hili linakwenda mtamboni, siyo Masauni wala Wambura waliopokea simu za waandishi wa Pambazuko, licha ya kutafutwa kwa siku mbili.

Jana, simu ya Wambura, ilipokelewa na msaidizi wake ambaye hakutaja jina na kusema Pambazuko limtafute Misime ambaye atazungumza, licha ya kuelezwa kuwa mwandishi anataka kuzungumza na Wambura binafsi.

Baada ya muda mfupi, wakati mwandishi anaendelea kusisitiza, akakata simu.



Mfanyabiashara Rostam Aziz

Habari



Mhadhiri wa Uchumi, Utafiti na Sera za Kimataifa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Bravious Kahyoza, akizungumza katika mahojiano maalumu na mhariri msanifu wa gazeti hili, Arodia Peter, kuhusu namna bora ya kushirikiana kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kutekeleza malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050. (Picha zote na Fidelis Felix)

Wachumi waeleza mazito Dira ya Maendeleo 2050

Na Arodia PETER

WATAALAM wa uchumi na biashara wamesema ufanisi wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050, inategemea zaidi ushirikiano wa sekta binafsi na umma.

Wakizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki kwa nyakati tofauti, wasomi hao walieleza kuwa Ubia wa Sekta Binafsi na Umma (PPP) utajenga nguzo imara za uendeshaji wa uchumi.

Mchumi na Mtafiti wa Sera za Kimataifa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. Bravious Kahyoza amesema uchumi imara msingi wake siyo kile kinachotokea ndani ya serikali, bali nje ya serikali.

Amesema kwa kipindi cha miaka 24 iliyopita, Tanzania imeweza kuchora na kutekeleza mipango, sera, na taratibu za kuyaendea maendeleo yake inayotegemea sekta ya umma kwa kiasi kikubwa.

Msomi huyo amesema katika kipindi hicho yamepatikana mafanikio katika maeneo mengi, huku ukuaji wa uchumi ukifikia aslimia 5.4 kwa wastani.

“Pamoja na mafanikio hayo, bado uchumi wetu siyo shindani, umaskini bado umeshamiri na maendeleo tuliyofikia bado siyo endelevu. Hii inahitaji kutafakari vizuri hatua inayofuata ambayo ni Dira ya 2050 na baada ya hapo,” alisema.

Aidha, mchumi huyo alishauri kuwa kwenye kutengeneza Dira ya Maendeleo 2050, mambo makuu manne ni muhimu kuzingatiwa.

Aliyataja mambo hayo kuwa ni pamoja na kurekebisha makosa ya kifalsafa ya kuendesha uchumi ambayo ni ukuaji wa uchumi unaotokona na sekta ya umma iliyo imara kwenye mazingira yenye sekta binafsi dhaifu.

Pia aliitaja kasoro nyingine kuwa ni kuamini kuwa uchumi ni kile kinachotokea serikalini, badala ya kile kinachotokea nje ya serikali.

Dkt. Kahyoza aliongeza kuwa unahitajika mkakati mahsusi wa kuzibadili rasilimali za asili kuwa rasilimali za kiuchumi.

Alisema Tanzania siyo tajiri kwa sababu ina rasilimali nyingi za asili, bali itakuwa tajiri siku ikiweza kuzibadili rasilimali hizo kuwa rasilimali za kiuchumi.

Mchumi huyo pia aligusia uanzishaji wa Kituo cha Ubia kati ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (PPP Centre) akisema kuwa hiyo ni hatua kubwa iliyochukuliwa na serikali.

Dkt. Kahyoza alipongeza hatua zilizoanza kuchukuliwa na mkurugenzi mkuu wa kwanza wa kituo hicho, David Kafulila, zinayoonesha umuhimu wa PPP.

Ili kufanya kazi hii njema iweze kwenda mbele zaidi kutahitajika mtazamo wa pamoja wa serikali, mifumo mizuri ya sheria, uhuru wa kitaasisi, tafiti za kutosha na kuongeza kasi katika kufungamanisha fikra za uchumi mpana na PPP Centre.

Inaendelea Uk. 35

Wachumi waeleza mazito Dira ya Maendeleo 2050

Inatoka Uk. 34

Mhadhiri mwingine wa UDSM, kutoka Shule Kuu ya Biashara, Dkt. David Rweikiza, amependekeza njia kadhaa za kuvutia uwekezaji nchini kuwa ni pamoja na kutambua umuhimu wa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma.

Amesema ni vyema Watanzania waelezwe wazi kwamba uchumi wa kijamaa siku hizi umebadilika, na kwamba huu siyo wakati serikali kumiliki njia kuu za uchumi.

Akitolea mfano, amesema China ambayo awali ilikuwa ya kijamaa, imebadilika kwa kuruhusu baadhi ya sekta kuendeshwa kwa ubia na sekta binafsi na zingine zinaongezewa mitaji ili ziwe na tija zaidi.

Dkt. Rweikiza aliongeza kuwa Tanzania ipo kwenye kipindi cha mpito kulinganisha kati ya uchumi wa kibepari na kijamaa, ingawa kinadharia Tanzaia inahitaji sekta binafsi na jukumu kubwa la serikali ni kuweka sera na kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kufanya shughuli zake.

"Mazingira mazuri ni pamoja na upatikanaji wa miundombinu muhimu ya umeme, usafiri na usafishaji, sheria rafiki, kodi himilivu na huduma za maji," ameongeza.

Kuhusu kuvutia mitaji nchini, mtaalam huyo wa biashara alishauri bajeti zote za miradi ya maendeleo zielekezwe kwenye PPP.

"Sekta na taasisi zilizo ndani ya serikali zijiandae kuipokea na kuanza kubuni miradi. kuhamasisha wananchi wajue umuhimu wa sekta binafsi, wanaoendesha hizi taasisi wajue umuhimu wake," akabainisha.

Mhadhiri wa Masuala ya Biashara wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro, Dkt. Frida Pacho amesema sekta binafsi inachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi.

Amesema sekta hiyo ni kinara wa uchumi kwa sababu inatoa ajira na kukuza na kuimarisha teknolojia ya ubunifu.



Mhadhiri wa Masuala ya Biashara wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro, Dkt. Frida Pacho



Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule Kuu ya Biashara, Dkt. David Rweikiza

Hata hivyo amesema licha ya serikali kujitahidi kurekebisha baadhi ya sheria ili kuvutia biashara na uwekezaji, bado juhudi zaidi zielekezwe kwenye kutengeneza miundombinu ikiwamo barabara ili kurahisisha usafirisaji.

"Kuwapo kwa mpango wa PPP ni juhudi za serikali katika kusadia sekta binafsi na biashara kwa sababu serikali haiwezi kufanya biashara," amesema na kusisitiza kuwa upo umuhimu hivi sasa kwa serikali kuboresha miundombinu ya Reli ya SGR na mazingira ya uwekezaji na biashara nchini.

Habari

Necta yapata dawa wizi wa mitihani



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mtihani (Necta), Said Mohamed

Na Mwandishi WETU

IMEKUWA kawaida kila mwaka matokeo ya darasa la saba, kidato cha nne na sita, yanapotangazwa lazima wawepo watahiniwa waliofutiwa matokeo, baada ya kubainika kufanya udanganyifu au kujihusisha na wizi wa mitihani.

Mwaka 2022 Baraza la Mitihani Tanzania (Necta), lilizifungia shule 24 kuwa vituo vya mitihani ya taifa baada ya kuthibitika kupanga kufanya udanganyifu katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi.

Shule hizo ambazo ni sawa na asilimia 0.13 ya vituo vyote vya mitihani nchini, ndani yake zipo shule maarufu ikiwemo ya Musabe ya jijini Mwanza na St. Anne Marie ya jijini Dar es Salaam na shule ya Rweikiza ya mkoani Kagera.

Nyingine ni Shule ya Msingi Kadama iliyopo Chato- Geita, Rweikiza (Bukoba), Kilimanjaro (Arusha) Sahare (Tanga), Ukerewe (Mwanza), Peaceland (Mwanza), Karume (Kagera), Al-hikma (Dar es Salaam).

Nyingine ni Kazoba (Kagera), Mugini (Mwanza), Busara (Mwanza), Jamia (kagera), Winners (Mwanza), , Elisabene (Songwe), High Challenge (Arusha), Tumaini (Mwanza), Olele (Mwanza), Mustlead (Pwani).

Pia zipo shule za Moregas (Mara), Leaders (Mara), Kivulini (Mwanza) na St. Severine (Kagera).

Vilevile mwaka 2023, jumla ya watahiniwa 31 walifutiwa matokeo kwa kufanya udanganyifu.

Kuendelea kujitokeza kwa tatizo hilo kila mwaka ni uthibitishio kuwa mamlaka husika zimeshindwa kupata mwarobaini wa tatizo hilo.

Kila mara mamlaka zimeeleza jitihada zinazochukulwia kukabiliana na hali hiyo, lakini hakuna matokeo ya kukomesha wizi huo.

Kutokana na hali hiyo, Necta sasa inakuja na mbinu mpya na madhubuti ya kukomesha wizi na kila aina ya udanganyifu kwenye mitihani.

Katibu mtendaji wa baraza hilo, Said Mohamed, alitoa tahadhari hiyo wiki iliyopita mbele ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wakati akitangaza maandalizi ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE).

Mtihani huo wa kumaliza elimu hiyo ya msingi ulifanyika kwa siku mbili Septemba 11 hadi 12, 2024.

Katibu huyo alisema jumla ya watahiniwa 1,230,780 walifanya mtihani huo, huku 564,176 sawa na asilimia 45.84 wakiwa wasichana na wavulana ni 666,604 sawa na asilimia 54.16.

Pia alisema watahiniwa wenye mahitaji maalumu waliosailiwa kufanya mtihani huo ni 4,583 kati yao 98 ni wasioona,1,402 wenye uoni hafifu, 1,067 wenye uziwi, 486 wenye ulemavu wa akili na 1,530 ni wenye ulemavu wa viungo.

“Kati ya watahiniwa 1,230,780 waliosajiliwa kufanya mtihani mwaka 2024, watahiniwa 1,158,862 sawa na asilimia 94.16 watafanya mtihani wa lugha ya Kiswahili na watahiniwa 71,918 sawa na asilimia 5.84 watafanya mtihani wa lugha ya Kiingereza ambayo wamekuwa wakiitumia katika kujifunzia,” alisema katibu huyo.

Kuhusu masomo waliotahiniwa, alisema ni sita ambayo ni Kiswahili, Lugha ya Kiingereza, Sayansi na Teknolojia, Hisabati, Maarifa ya Jamii, Stadi za Maisha na Uraia.

CWT kujadili kusitishwa kwa mtaala mpya



Rais wa CWT, Leah Ulaya

Na Elizabeth HOMBO

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimepanga kuwakutanisha wadau wake kujadili mabadiliko yaliyotangazwa na Wizara ya Elimu kuhusu mabadiliko ya mtaala mpya wa kidato cha tano.

Rais wa CWT, Leah Ulaya, ameliambia Pambazuko mwishoni mwa wiki kuwa lengo ni kupata msimamo wa chama hicho kutokana na mabadiliko hayo ambayo yalitangazwa hivi karibuni na Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda.

"Tunakaa na wadau ili tutoe majibu yaliyo sawa, halafu tutawafahamisha," alisema Ulaya.

Katika tangazo hilo, Prof. Mkenda alitangaza kusitishwa kwa baadhi ya tahasusi mpya zilizoanzishwa kwa ajili ya wanafunzi waliojiunga na kidato cha tano mwaka huu.

Suala hilo limewagawa wadau wa elimu huku baadhi yao wakieleza kuwa mabadiliko hayo yanaweza kuziathiri baadhi ya shule ambazo zilifanya uwekezaji kama maandalizi ya kuanzisha tahasusi hizo mpya.

Katika tamko alilolitoa kwa waandishi wa habari Julai 25, 2024 jijini Dodoma, Prof. Mkenda alisema matumizi ya mtaala mpya yamesitishwa kwa sababu ya changamoto za kiufundi, ikiwemo kuchelewa kuchapishwa kwa nakala ngumu za vitabu.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Shule Binafsi (Tamngosco), Aman Lyimo, amesema wao hawaoni kama uamuzi huo una madhara sana, kwa sababu matumizi ya mtaala huo umeahirishwa kwa mwaka mmoja tu.

Akizungumzia kuhusu shule ambazo zilifanya uwekezaji ikiwa ni maandalizi ya utekelezaji wa mtaala huo, ikiwamo kuajiri walimu, alisema haoni tatizo kwa sababu hakuna mwalimu ambaye amejikita kwenye somo moja tu.

"Sioni kama kuna madhara na naona uamuzi huu wa wizara umetupa nafasi ya kujipanga zaidi. Athari zinaweza kuwepo kwa wale ambao walijiandaa na pengine wakachukua mkopo, ndiyo itakuwa changamoto kidogo kwao," alisema Lyimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Elimu (TET), Dkt. Annet Komba, alisema hakuna atakayepata madhara na kwamba waziri aliweka wazi kila kitu.

"Mimi sioni kama kuna tatizo kwa sababu waziri alieleza vizuri sana," alisema Dkt. Komba huku akimtumia mwandishi wa habari hizi picha jongefu za tamko la Waziri Mkenda kupitia WhatsAPP.

Mhadhiri wa Elimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. George Kahangwa aliliambia Pambazuko kuwa mabadiliko hayo hayana madhara kwa sababu tahasusi nyingi ni zilezile za zamani.

"Ndiyo maana wanafunzi wameweza kuendelea na masomo licha ya kwamba mtaala mpya umesitishwa," alisema.

"Kama kuna ambao wamepata madhara, sasa wana wajibu wa kutoa ripoti pengine hata kudai fidia kwa sababu sheria za nchi zipo. Hapa ni suala la wamiliki wa shule kutathimni hasara waliyoipata," aliongeza.

Hata hivyo, Dkt. Kahangwa amesema pamoja na maboresho haya yanayofanyika, lakini serikali ijifunze kujipa muda kabla ya kuanza rasmi kwa mabadiliko.

Habari

Wahimizwa ‘kuchangamkia’ bima



Siku ya Bima ya mwaka huu jijini Dodoma, ilitanguliwa na matembezi yaliyofanyika kwa kujumuisha wafanyakazi wa kampuni za bima, mawakala na madalali wa bima. Katika picha hii wanaonekana baadhi ya wafanyakazi kutoka Howden Insurance Brokers. (Picha na Mpigapicha Maalum).

Na Mwandishi WETU, Dodoma

PAMOJA na umuhimu mkubwa wa bima kwa Watanzania, bado mwamko kwa wananchi ni mdogo kuhusu huduma hiyo.

Ingawa hali ya mwamko huo ni mbaya zaidi maeneo ya vijijini, bado hata mijini, kuna idadi ndogo ya watu wanaotumia huduma za bima, ikiwamo za afya, nyumba, bidhaa, safari, majanga na nyingine nyingi.

Kidogo, kwa wale walioko mijini, bima pekee inayozingatiwa ni ile ya magari na vyombo vingine vya moto, kwa kuwa tu inalazimishwa na sheria za nchi.

Ni kutokana na sababu hiyo, wadau wa sekta ya bima Tanzania wamekuwa wakikutana kwa ajili ya kujadili na kuzungumza namna nzuri ya kuhamasisha wananchi “kuchangamkia” huduma za bima ili kujilinda dhidi ya madhila mbalimbali yanayoweza kutokea.

Mtaalamu wa bima ambaye ameshiriki mkutano wa mwaka huu wa Siku ya Bima, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita, Comfort Mkina, amesema wakati umefika sasa kwa Watanzania kutambua umuhimu wa kila mtu, kila familia kuwa na bima za aina mbalimbali ili kupata nafuu kila wanapokumbwa na majanga.

Comfort, ambaye ni ofisa kutoka Kampuni ya Bima ya Howden, amesema huduma za bima ni mkombozi na msaidizi muhimu wa ulinzi, hivyo ni vyema “kukumbatiwa” na kila mtu, kampuni na taasisi zote.

Mkutano wa kila mwaka wa Siku ya Bima ulifanyika – Jumamosi, Septemba 14, 2024 jijini Dodoma. Wadau mbalimbali katika sekta ya bima wamekutana ambapo Mgeni Rasmi ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum Dkt. Dorothy Gwajima.

Mkutano huu ni mwendelezo wa Wiki ya Bima 2024 na uliandaliwa na Taasisi ya Bima (IIT) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ukiwa na lengo la kukutanisha wadau wa bima wakiwemo kampuni za bima, vyuo, taasisi za bima na watumiaji wa huduma za bima, kujadili mambo mbalimbali kuhusu sekta ya bima nchini.

Katika hotuba yake, Dkt. Gwajima aliipongeza TIRA kwa majukumu ya kutoa elimu ya bima kwa Watanzania na kusisitiza elimu ya bima kutolewa zaidi kwa jamii.

Dkt. Gwajima pia alisisitiza kauli mbiu hii ya mwaka huu “Bima Jumuishi: Bidhaa Zinazokidhi Mahitaji na Usambazaji wa Kiteknolojia” - ikawafanye wadau kuwa na tafakuri ya mpango mkuu wa maendeleo ya sekta ya fedha 2020 – 2030 kwa sekta ndogo ya bima, sambamba na maelekezo ya serikali.

Dkt Nchimbi: Nchi inapitia kipindi kigumu



Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi

Na Mwandishi WETU

UTEKAJI, utesaji na mauaji, yanayoonekana kushika kasi nchini kwa sasa, yamekiibua Chama Cha Mapinduzi (CCM) kukemea, huku kikieleza kuwa "nchi inapitia kipindi kigumu."

Katika mkutano wake na wanahabari Ijumaa iliyopita, Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi alisema amelazimika kutoka hadharani kuweka wazi msimamo wa chama hicho, kutokana na kukerwa na matendo hayo.

Alisema chama chake, kitahakikisha kinatimiza wajibu wake ipasavyo, kwa kupaza sauti na kuchukua hatua kukomesha vitendo hivyo.

Dkt. Nchimbi aliainisha kuwa kwa sasa nchi inapitia kipindi kigumu, kwani matukio ya utekaji na mauaji, hayana tofauti na vipindi vigumu ambavyo taifa limepitia katika uhai wake wa miaka 60, ikiwemo Vita ya Kagera, matukio ya ukame na njaa, mapambano ya vita vya ukombozi kusini mwa Afrika na ugonjwa wa Covid-19.

"Sasa taifa letu linapita katika changamoto kubwa ya hofu miongoni mwa wananchi, ambayo hatuwezi kuipuuza, ni lazima tuizungumzie kwa sababu pia ni sehemu ya maelekezo ya Ilani ya CCM, inayoeleza kuwa moja ya mambo ya kufanya ni kulielekeza Jeshi la Polisi kutekeleza wajibu wake kwa uadilifu.

"Kwa vyovyote vile, suala la amani, utulivu, usalama wa raia na mali zao, ni moja ya ahadi muhimu za CCM kwa raia ambao utekelezaji wake unasimamiwa na Jeshi la Polisi..."

"Mtu yeyote anayehatarisha usalama wa raia, anayeshiriki kuteka raia, anayeshiriki mauaji ya raia au kikundi chochote kinachosababisha raia kuishi kwa hofu, ni wazi yanafanyika haya kuharibu taswira ya CCM mbele ya umma,"alisema.

Kiongozi huyo akitumia mkutano na waandishi wahabari "kukisafisha chama chake," alisema CCM inahusishwa na matukio hayo kwa kuwa baadhi ya viongozi wake wanatoa kauli za "ajabu-ajabu" ambazo hazina uhusiano na chama hicho tawala.

Dkt. Nchimbi alisema CCM inaunga mkono kauli ya Rais Samua Suluhu Hassan aliyoitoa kukemea vitendo vya kuteka, kutesa na kuua raia wasiokuwa na hatia.

Kauli ya Rais Samia, kupitia mtandao wa X, aliandika kukemea vitendo hivyo, huku akilitaka Jeshi la Polisi kuhakikisha wahusika wa kuteka, kutesa na kuua kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mohammed Ali Kibao wanapatikana na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Dkt. Nchimbi alieleza kuwa anatambua msingi wa amani katika nchi ni haki, ambayo ni lazima ionekane inalindwa kwa kuvishajihisha pia vyombo vya sheria kwa nguvu zao zote na inapofika suala la kutenda haki kusiwe na muhali.

"Ni lazima tufanye kila njia kuhakikisha kama taifa kila mtu anatendewa haki, tuhakikishe yeyote anayetuhumiwa kwa kosa asionekane mkosaji hadi uthibitisho unatolewa, na sisi CCM tutataka kila inavyowezekana demokrasia nchini iendelee kushamiri, mahusiano ya vyama yaendelee kuimarika na tuendelee kuijenga nchi yetu," alisisitiza.

Habari



Mchezaji wa zamani wa Arsenal, Nwankwo Kanu (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Upasuaji, Dkt. Godlove Mfuko (kulia) alipotembelea Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na MNH)

Kanu afagilia Hospitali ya Muhimbili

Na Mwandishi WETU

SIFA, umaarufu na umuhimu wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili unazidi kudhihiri duniani, kwa kuwa watendaji wake wamesheheni weledi, utu na kujituma.

Pamoja na mambo mengine, hospitali hiyo imekuwa kimbilio siyo kwa Watanzania tu, bali majirani kutoka nchi za Uganda, Kenya, Malawi, Zambia na hata DR Congo ambao wamekuwa "wakifurika" kupata huduma za kibingwa.

Hospitali ya Muhimbili ndiyo inayoongoza kwa kupata watalii wanaofika Tanzania kwa ajili ya tiba, ushauri na shughuli zingine za kitabibu.

Ni kutokana na sifa hizo, watu mashuhuri kutoka maeneo mengi ya dunia, wamekuwa wakifika Hospitali ya Muhimbili kujifunza na kuona mzizi wa sifa na umaarufu wa hiospitali hiyo ya Tanzania.

Miongoni mwa wageni mashuhuri waliotembelea Muhimbili hivi karibuni ni mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Nigeria na Arsenal ya England, Nwankwo Kanu.

Wiki iliyopita, Kanu alitembelea Hospitali ya Taifa Muhimbili -Mloganzila kwa lengo la kuwajulia hali na kuwafariji wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo na kuangalia maeneo wanayoweza kushirikiana.

Kanu ambaye ni mwanzilishi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Kanu Heart Foundation ametembelea kitengo cha uchunguzi wa magonjwa ya moyo, wodi ya kulaza wagonjwa ya moyo pamoja na kutembelea wodi ya watoto wanaopatiwa joto na mama zao kufuatia kuzaliwa wakiwa na uzito mdogo maarufu kangaroo.

Kanu ambaye aliwaji kufanyiwa upasuaji wa moyo, amebainisha kuwa taasisi yake imeshatoa ufadhili wa matibabu ya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa 90 kutoka Tanzania ambao walisafirishwa kwenda India kwa atibabu.


Nyota huyo wa mpira wa miguu, aliwapongeza watoa huduma wa afya kwa kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa watu wanahudumiwa na kurejea katika hali zao za awali.

Akiongea kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Upasuaji, Dkt. Godlove Mfuko alisema Muhimbili - Mloganzila inahudumia takribani wagonjwa 1,000 kwa siku, kati ya hao wenye changamoto za moyo ni takribani 60.

Dkt. Mfuko aliongeza kuwa kupitia mpango wa Samia Scholarship, hospitali hiyo imeendelea kunufaika kwa kuendelea kutatua changamoto za upungufu wa watumishi, hususan katika eneo la magonjwa ya moyo.

Kanu amewasili Tanzania nchini kwa uratibu wa Vodacom Foundation ambao kwa pamoja mwaka huu wanafadhili mashindano ya kuendesha baiskeli 'twende Butiama' yenye lengo la kukusanya fedha kusaidia jamii, ikiwa ni maadhimisho ya miaka 25 ya kifo cha Baba wa Taifa, Julius Nyerere ambaye alipambana na ujinga, maradhi na umasikini.

Askofu Sendoro kuzikwa kesho



Na Mwandishi WETU

MWILI wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Jimbo la Mwanga, Dkt. Chediel Sendoro, unatarajiwa kuzikwa kesho, ikiwa ni sehemu ya kuhitimisha ibada yake ya mwisho duniani.

Askofu Sendoro alifariki dunia kwa ajali ya gari iliyotokea katika eneo la Kisangiro, Kilimanjaro Septemba 9, 2024.

Taarifa iliyotolewa na familia, mwili wake utatolewa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini, KCMC leo Jumatatu, Septemba 16, 2024 na kupelekwa kwenye Kanisa Kuu Mwanga ambapo taratibu za kutoa heshima za mwisho zitaanza saa 4 asubuhi, zikishirikisha waumini na watu wote.

Familia imeeleza kuwa baada ya ibada maalumu na taratibu zote za kuuaga mwili huo na kutoa heshima za mwisho, mwili huo unatarajiwa kuzikwa kesho utazikwa katika Kanisa Kuu la Dayosisi ya Mwanga.

Askofu Sendoro alifariki dunia Septemba 9, 2024 kwa ajali ya gari iliyotokea majira ya saa 1:30 usiku baada ya gari alilokuwa akiendesha, aina ya Toyota Prado, akitokea Kileo kuelekea nyumbani Mwanga, kugongana uso kwa uso na lori.

Askofu Sendoro ndiye askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Mwanga ambaye aliingizwa kazini Jumapili ya Novemba 6, 2016, baada ya kuzaliwa kwa dayosisi hiyo mpya iliyotokana na kugawanywa kwa dayosisi mama ya Pare baada ya mgogoro uliodumu kwa miaka mingi.

Akimzungumzia askofu huyo, msemaji wa familia ambaye ni kaka wa marehemu, Jeremiah Sendoro, alisema Askofu Sendoro alikuwa mtu wa Kanisa, familia na jamii na katika maisha yake alimuweka Mungu mbele katika kila jambo.

Alisema watamkumbuka katika mambo mengi, lakini kubwa ni upendo na ushirikiano wake kwa familia na jamii yote iliyomzunguka, ambapo katika shughuli za familia alishiriki kama mwanafamilia na hakuwahi kuinua mabega kuonyesha kwamba yeye ni askofu.

Akizumzungumzia Askofu Dkt. Sendoro, Askofu wa KKKT Dayosisi ya Pare, Charles Mjema, alisema msiba huo umemgusa zaidi kwa kuwa licha ya askofu huyo kuwa mtenda kazi mwenzake pia alikuwa rafiki yake.

Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Mwanga, Mchungaji Timoth Msangi alisema msiba huo ni pigo kwao kwa kuwa wamempoteza kiongozi shupavu na mashuhuri aliyesimama kuijenga dayosisi hiyo na kuhakikisha kazi ya Mungu inasonga mbele.

Habari

Suluhu migogoro ya ardhi Morogoro sasa yapatikana

Na Mwandishi WETU

MIGOGORO sugu ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji katika vijiji vya wilaya nne za Mkoa wa Morogoro, imepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Hatua ya kudhibiti migogoro hiyo imefanikishwa na shirika lisilo la kiserikali la Helvetas-Tanzania kwa kushirikiana na taassi zingine, kuwezesha programu ya upimaji na matumizi bora ya ardhi.

Wilaya zilizonufaika na programu hiyo ni Morogoro Vijijini, Ulanga, Malinyi na Mvomero.

Programu hiyo ni sehemu ya mradi wa uhifadhi wa mazingira unaoitwa Uwezeshaji Jamii katika Usimamizi Endelevu wa Misitu na Nishati Mbadala (Usemini) unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Umoja wa Ulaya (EU) umetoa asilimia 90 ya bajeti ya mradi ya kiasi cha zaidi ya Euro milioni 2.2 na asilimia 10 imetolewa na shirika la Helvetas.

Wadau wengine wa mradi huo wa ni mashirika ya Codert na Mjumita.

Mradi huo pamoja na uhifadhi wa mazingira, nishati mbadala, pia utahusisha upandaji miti ya kawaida na matunda zaidi milioni tano.

Akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea maendeleo ya mradi huo mwishoni mwa wiki, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kinonko, Wilaya ya Morogoro Vijijini, Juma Shaban, alieleza kuwa baada ya kuanzishwa kwa mradi huo, migogoro ya ardhi kijijini hapo imeanza kupungua.

Shaban alisema anaamini kuwa kupitia mradi huo, migogoro ya ardhi baina wakulima na wafugaji, itakuwa imepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Alisema kabla mradi huo, ofisi ya kijiji ilikuwa inapokea kesi na malalamiko ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji pamoja na watu binafsi zaidi nne kwa siku.

Ofisa huyo alieleza kuwa baada ya ardhi ya kijiji hicho kupimwa, wametenga maeneo kwa ajili makundi yote kufanya shughuli mbalimbali pamoja na misitu. “Tumetenga maeneo kwa ajili ya shughuli za makazi, ufugaji, kilimo na tumetunga sheria ndogo ndogo ili watakaokiuka na kuvamia maeneo ya wengine, wachukuliwe hatua,” alisema.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Hamidu Gamba, alisema kabla ya programu hiyo, migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji ilisababisha mapigano ya mara kwa mara, hasara ya upotevu wa mali na maisha ya watu.

“Kwa sasa baada ya kupungua kwa migogoro wakulima na wafugaji, hali ya amani katika jamii imerejea na shughuli za kiuchumi zinaendelea kwa makundi yote,” alisema.


Mkuu wa Wilaya Ulanga, Dkt. Julius Ningu, alisema katika wilaya yake, program hiyo imeleta manufaa makubwa baada ya vijiji vyote 58 kupimwa na kutenga maeneo ya shughuli za kichumi kwa watu wote pamoja na maeneo ya makazi.

Mratibu wa mradi huo wa Usemini, Daniel Kalimbiya, alisema baadhi ya faida za mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa jamii ni pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali ardhi, kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

“Faida nyingine ni kuondoa migogoro ya ardhi baina watumiaji wa ardhi, kusaidia utunzaji wa ardhi, hasa vyanzo vya maji, kuzuia ufyekaji wa misitu na mapori yaliyohifadhiwa kwa matumizi maalumu,” alisema Kalimbiya.

“Pia kuwezesha matumizi endelevu ya ardhi na rasilimali zake, kutokana na kupangilia rasilimali hizo kulingana na mahitaji ya makundi mbalimbali ya kijamii na kuepuka mwingiliano wa kimatumizi baina ya makundi.”

Kalimbiya alisema mradi huo utakapofikia tamati mwaka 2026 wanatarajia kupanda miti zaidi ya milioni tano na wanufaika 10,000 kutoka kaya 2,000.





Na Hellen NGOROMERA

Kinachokera wanawake wengi kwenye uhusiano - 1

KARIBU msomaji wa safu ya uhusiano, ambapo wiki iliyopita nilizungumza kuhusu mambo yanayowakera wanaume kwenye maisha ya ndoa au uhusiano, na leo naendelea na mada hiyo, lakini nikigeukia upande wa yale yanayowakera wanawake.

Mwanamke ni kiumbe anayependa kupendwa, kujaliwa na kutimiziwa mambo anayoyataka. Mambo hayo ndio msingi mkuu kwake.

Wanawake wamekuwa wakiumizwa na mambo mengi kutoka kwa waume zao au rafiki zao katika uhusiano jambo ambalo limesababisha wengi kushindwa kufurahia maisha hayo na kusababisha migongano.

Hivi karibuni nilimsikia mtaalamu mmoja wa masuala ya uhusiano na ndoa akizungumza mtandaoni kwamba mwanamke hata apewe gari au vitu vingine vya kifahari, usipodhihirisha upendo wako kwa maneno, hawezi kukuelewa na kusadiki kuwa unampenda.

Alisema mwanamke hutaka kuelezwa na mpenzi wake kuwa anapendwa kila saa, pia anataka apewe ulinzi kwenye mapenzi, kufarijiwa na kuenziwa; hiyo ndiyo faraja kwake.

Alitaja jambo lingine linalomumiza mwanamke kuwa ni tabia ya ubahili kwa mwanaume na kukwepa majukumu ya familia anayoiongoza.

"Ubahili wa mwanaume hata katika masuala muhimu ya watoto wao, ikiwemo elimu kunamchukiza mwanamke na jambo hilo linaweza kusababisha kuchepuka au kuachana na mwenza wake au mumewe ikiwa atampata mtu ambaye atampa fedha," alisema.

Ni wazi kwamba mwanamke anapoolewa huungana na mumewe akitarajia kuwa mume ndiye atabeba gharama zote za kuitunza familia.

Wanaume wanapaswa kufahamu kuwa riziki zao kutoka kwenye shughuli zao, zitaongezeka ikiwa watatimiza majukumu yao vyema kwa wake na watoto, kwani hao ndio baraka kuu kwao.

Kikubwa kinachopaswa kuzingatiwa na mwanaume na mwanamke, ni upendo wa dhati kati yao.

Tukutane wiki ijayo.



Kwa maoni na ushauri: hellen-2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

‘Boyfriend jinzi’ bado zinatamba

FASHENI ya suruali za jinzi bado “inabamba” sana, na uhakika ni kwamba inapendeza kwa wengi.

Kuna aina nyingi za vazi hilo na kutokana na kupendwa, kuna majina mengi kuhusu jinzi; ikiwamo skinny jinzi, mom jinzi, cargo na boyfriend na nyinginezo.

Leo nazungumzia boyfriend jinzi ambazo kwa mwonekano huwa ni pana kuanzia juu hadi chini, lakini zinapendeza zikivaliwa.

Jinzi hizi hakika zinapendeza hasa kwa wadada au wanawake wenye umbo la pembetatu (ipo siku tutajifunza kuhusu maumbo ya miili yetu), ambao wana hipsi ndogo kuliko mabega pamoja na wenye umbo la yai, bila kusahau wale wenye mstatili.



Suruali hizi zinapendeza zikivaliwa na crop top ama top ambayo ni ndogo inayoshika mwili.

Pia zinavutia iwapo utaongezea na koti ambalo unaliegesha tu mabegani au unalivaa pasipo kufunga vishikizo.





Tumia sukari, mafuta mnyonyo kulainisha mikono

KUNA sababu nyingi za kuifanya mikono kuwa migumu, mojawapo ikiwa ni matumizi ya sabuni hususani ya unga.

Hapa nimekuwekea namna bora ya kuifanya mikono kuendelea kuwa laini.

Tumia mafuta mnyonyo na sukari. Changanya mchanganyiko huo kisha pakaa kwa kusugua taratibu mikono yote kuzunguka kiganja kizima.

Tumia dakika kumi kwa zoezi hili kisha nawa na maji ya uvuguvugu.

Pakaa mafuta yako ya mikono na endelea na shughuli nyingine.

Fanya zoezi hili angalau mara tatu kwa wiki.

Kwa maoni na ushauri: piga simu 0656531217

Afcon



Mbungi imeonekana, bado kazi ipo

Na John MARWA

WAKATI Tanzania, Kenya na Uganda zikiwa kwenye maandalizi jadidi ya kuandaa Fainali za Mataifa ya Afrika 'Pamoja Afcon 2027' nje ya Uwanja na miundombinu yote inayohitaji, Ndani ya uwanja mambo yanachagiza mwendo wao.

Juma lililopita ishuhudia mitanange ya kuwania kufuzu Afcon 2025 itakayopigwa nchini Morocco, ambapo mataifa yote matatu yameanza vyema kampeni zao kuelekea Morocco kabla ya wao kuwa wenyeji.

Tanzania, Kenya na Uganda zilishuka viwanjani katika makundi yao ya kuwania kufuzu fainali hizo ambazo watakabidhiwa bendera ya uenyeji kwenye fainali zinazofuata kila timu imeonyesha njaa na sababu za kuelekea huko.

Tanzania katika Kundi H, Taifa Stars ilicheza michezo miwili na kufanikiwa kuvuna pointi 4, ikitoka suluhu dhidi ya Ethiopia nyumbani na kwenda kuchukua alama tatu ugenini dhidi ya Guinea.

Matokeo ambayo yameiweka nafasi ya pili nyuma ya DR Congo wenye pointi 6, Ethiopia pointi moja huku Guinea wakiburuza mkia na kila timu ikiwa na michezo minne mkononi.

Kwa matokeo hayo, Stars inahitaji alama zisizopungua 5 kati ya 12 zakupambania ili kujihakikishia kufuzu Afcon 2025; ambapo wana michezo miwili nyumbani na miwili ugenini.

Kwa upande wa Kenya, nao hawajaanza kinyonge wakiwa Kundi J, wao ndio vinara wa kundi na pointi zao 4 sawa na Cameroon ambapo wametoka sare moja na kushinda moja kundi ambalo linazijumuisha Zimbabwe na Namibia.

Kenya ilitoka suluhu dhidi ya Zimbabwe kisha kuwachapa Namibia mabao 2-1, kibarua kinachofuata ni kuwavaa Cameroon katika michezo miwili inayofuata.


Nao Uganda waliandikisha pointi 4 kwenye Kundi K, sawa na waambata wenzake, Tanzania na Kenya, ambapo walitoka sare ya 2-2 dhidi ya Afrika Kusini na kushinda 2-0 dhidi ya Congo Brazaville.

Uganda wanayo nafasi kubwa kufanya vizuri kwani mshindani wao mkubwa ni Afrika Kusini ambaye wameshacheza naye mchezo mmoja na hivyo kuwa na kibarua dhidi ya Sudan Kusini katika michezo miwili inayofuata.

Ukitazama matokeo hayo kwa timu zote tatu, kuna ishara ya kufuzu kama kazi ya ziada itafanyika katika viwanja vya mazoezi na maandalizi ya kuzicheza hizo mechi nne zilizosalia bila kujali ugumu wa wapinzani wao.

Pointi nne kwa kila nchi ni wazi hii ndio maana ya "Pamoja Afcon 2027" – hivyo kuonyesha kuwepo kwa kiu ya kusafisha njia ya kuifikia zamu yao ya kuwa wenyeji.







Dimpoz afunguka sakata la kukwepa bili ya WCB

Dar es Salaam, Tanzania

MSANII wa Bongo Fleva, Omari Nyembo maarufu kama Ommy Dimpoz amefunguka sakata la kuonekana kwenye video fupi inayomuonyesha akikwepa kulipa bili ya vinywaji vilivyotumiwa na wasanii wa lebo ya Wasafi (WCB).

Sakata hilo limetokea kwenye hafla iliyoandaliwa na WCB Wasafi hivi karibuni ambapo alikuwa mgeni mualikwa.

Baada ya waandishi kutaka kujua kwa kina kuhusu sababu za kukwepa bili hiyo, Dimpoz aliishia kujibu swali hilo kwa kumuuliza mwandishi kuwa "wewe unaweza kuihudumia wasafi wote, ndio nilikuwa nakwepa pale unataka niseme sio mimi yule, ni mimi na nilikuwepo".

Alipoulizwa kuwa ile bili ilikuwa ya bei gani, alijibu "ni kama milioni sita hivi.

"All in all' mimi nilikuwa mualikwa, hivyo lazima ujue. Ukishakuwa mualikwa maana yake 'everything' (Kila Kitu) ilikuwa 'under' (chini) yao ila sasa muhudumu aliamua kuniteua mimi ndio maana Onesmo (mlinzi wa Diamond), aliamua kunipora na kuipeleka kwa muhusika sasa kwa nini nilipe mimi, alihoji tena na kusema mimi ni nani? halafu sasa unaanzaje kulipa mbele ya tajiri namba moja duniani. Huu ni ukosefu wa adabu, nilimuachia tajiri alipe na alimaliza.

Alikiba kutikisa na EP yake mpya

Dar es Salaam, Tanzania

MFALME wa Bongo Fleva Alikiba ameshea taarifa fupi kuhusu ujio wa Extended Play 'EP' yake mpya inayokwenda kwa jina la "Starter," akisema itakuwa mwanzo wa safari yake ya kimuziki inayogusa hisia za maisha halisi.

Alikiba amegusia kuwa kila wimbo kwenye EP hiyo unatoa fursa ya kuingia kwenye vipengele mbalimbali ikiwemo upendo, ukuaji na kujitambua ikiwa na midundo ya kuvutia, mashairi ya kugusa moyo na mapigo ya kipekee.

EP hiyo itaachiwa rasmi Septemba 20, ikiwa na nyimbo 7, tatu zikiwa ni kolabo ya Nandy, Marioo na Jay Melody.



Drake aweka rekodi ya kibabe

New york City, Marekani

HII sasa sifa, hivi ndivyo unavyoweza kusema kwa rapa Aubrey Gharam 'Drake' baada ya kuweka rekodi ya kuwa msanii wa kwanza kuuza nakala zaidi ya milioni 5 za albamu zake nchini Marekani kwa mwaka huu (2024).

Ikumbukwe hadi sasa rekodi hiyo inashikiliwa na yeye pekee na hakuna msanii mwingine ambaye amefika hata mauzo ya nakala milioni 3.5 kwa mwaka huu.



Arsenal waiteka London kibabe

LONDON, ENGLAND

MOJA ya mchezo bora ulishuhudiwa wikiendi iliyoisha jana ni London Derby, ambapo Tottenham Hopsurs waliwaalika 'The Gunners' – Arsenal.

Katika mchezo huo uliojaa burudani kutoka makocha wa pande zote mbili licha ya vijana wa Mikel Arteta kuondoka na ushindi wa bao 0-1.

Haikuwa rahisi kwa vijana wa Arsenal, lakini umahiri wa Arteta kujua sifa za wachezaji wa timu pinzani, kujua nini wanaweza kufanya katika mazingira fulani uwanjani ili kuja na mpango kazi sahihi wa ushindi ndiyo ulioipa ushindi timu yake.

Arteta aliamua kufunga njia za ndani akifahamu fika moja ya silaha kubwa ya Spurs ni pasi za ndani na Arsenal walipabana sana kuhakikisha wanavuruga na kupora mipira ya wapinzania wao, kisha kuutanua uwanja wakati wanashambulia kwa kuwatumia zaidi Saka na Martinelli.

Wakati huohuo, Arteta alifahamu akiwalazimisha Spurs kutanuka wakati wa kushambulia, akiamini walinzi wake kupambania mipira ya juu, ni chakula chao akina Saliba, Gabriel na Raya ambao walitafsiri vyema maarifa ya Arteta.

Dakika ya 64 mlinzi raia wa Brazili aliandikia Arsenal bao la kuongoza, na la ushindi na mitutu ikaitika kwa risasi moja kuelekea ka Spurs. Bao hilo lilidumu hadi dakika ya mwisho ya mchezo.

Matokeo hayo yanaifanya Arsenal kuendelea kusalia nafasi ya pili kwenye msimamo wa EPL na pointi zao 10, michezo minne, wakishinda mitatu na sare moja nyuma ya vinara Manchester City ambao wameshinda michezo yote minne msimu huu pointi 12.

MICHEZO

Jumatatu, Septemba 16-22, 2024



Kiungo wa Simba, Edwin Balua akijaribu kumtoka mchezaji wa Al Ahly Tripoli ya Libra katika mchezo uliochezwa jana nchini humo ambapo ulimalizika kwa sare 0-0. (Picha na Simba)

Yanga gia imekubali, Simba kama kawa

Na John MARWA

TIMU ya Yanga, almaarufu 'Wananchi' imeendelea na safari ya matumaini kusaka kibali cha kurejea kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF CL) kwa msimu wa pili mtawalia kwa kupata ushindi wa bao 0-1 ugenini dhidi ya CBE SA ya Ethiopia mchezo wa mkondo wa kwanza hatua ya awali.

Bao la Yanga liliwekwa kambani na Prince Dube dakika za mwisho kipindi cha kwanza na kuwafanya Wananchi kurejea na mtaji wa bao la ugenini.

Ulikuwa mchezo ambao Kocha Miguel Angel Gamondi aliuweka kwenye kiganja chake kwa namna ambavyo aliutawala kwenye maeneo mengi ya uwanja, huku vijana wake wakikosa ufanisi wa kumalizia nafasi nyingi walizozitengeneza.

Yanga wanaonyesha kuwa imara sana, lakini kuna ufanisi wameupoteza kwa kiwango kikubwa baada yakurejea kutoka kwenye kalenda ya FIFA.

Umakini unahitajika zaidi maana mchezo wa soka hauna simile ukishindwa kutumia nafasi vizuri.

Mchezo wa mkondo wa pili utapigwa wikiendi hii Septemba 21, ambapo Yanga watawaalika CBE huko Zanzibar kwenye Dimba la New Amani Complex kumalizia kazi walioianza.

Wakati wananchi wakiendeleza moto wa kuondoka na ushindi katika viwanja mbalimbali Afrika, watani zao, Simba, nao kazi imeanza ambapo shughuli imeanzia nchini Libya kusaka tiketi ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Simba, almaarufu – 'Mnyama' alishuka dimbani nchini Libya dhidi ya Al Ahli Tripoli ambao wameonekana kuwa bora sana kwenye dirisha la usajili wakiwa wanajitafuta kurejea kwenye makali yao.

Lakini, hadithi mbaya kwa Walibya hao ni kuwa wameingia kwenye mdomo wa Mnyama ambaye kwa misimu mitano mtawalia, amecheza hatua ya makundi na kutinga robo fainali.

Shauku ya vijana wengi wenye vipaji vikubwa kuvaa uzi wa Mnyama inaweza kuwa silaha ya Wekundi hao wa Msimbazi kuendeleza mishemishe zake za kutoa pumzi ya moto katika michuano ya Afrika.

Ni mchezo ambao ni wa kwanza kwa Kocha Fadlu Davis ambaye amebeba matumaini makubwa kwa Wanasimba ambao wako katika karakana ya kuunda jeshi lao jipya katika uwanja wa mapambano.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION